MSTAHIWA SHEIKH AHMAD BIN HAMAD
AL KHALILI
MUFTI MKUU WA OMAN

Kuondoa Utata Uliyomo katika Tafauti ya Muandamo

[Kauli za Maulama wa Madhehebu Nne]

Imefasiriwa kwa Kiswahili na:
Munir Sulaiman Aziz Al Masrouri
1431AH/2010CE

Jawabu maalumu kwa mwenye kutatizwa na tafauti ya muandamo wa mwezi baina ya nchi za Kiislamu na athari yake katika kuanza na kumaliza kwa Mwezi wa Ramadhani, siku ya kusali Sala ya Idi, Saumu ya Arafa na Kuchinja Udh'hiya.

بسم الله الرحمن الرحيم

DIBAJI

Shukrani zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema; kailimisha Qur'ani akaikamilisha neema; kamuumba mtu katika umbo kamilifu, akumfundisha kunena kwa ulimi bainifu. Na rehma na amani zimshukie Mbora wa viumbe Vyake, Hitimisho la Manabii na Mitume Yake – Muhammad, pamoja na Aali zake, na Sahaba zake, na kila aliye ongoka kwa uongofu wake, akufuata njia yake hadi Siku ya Malipo.

Asili ya kitabu hiki ni jawabu maalumu ya Mstahiwa Sheikh Ahmad bin Hamad Al Khalili, Mufti Mkuu wa Oman, kwa barua aliyotumiwa na mmoja wa wasomi wanao heshimika katika jamii. Madhumuni ya barua hiyo ilikuwa kuhoji uamuzi wa Oman wa kuto kufuata muandamo wa Ummul-Qura (Makka Al-Mukarrama) wa mwezi wa Dhul-hijja kama ilivo katika nchi za jirani.

Mwenye barua ana uoni wa kwamba nchi zote za Kiislamu ingepasa zifuate muandamo wa Ummul-Qura kwa mwezi wa Dhul-hijja, kwa kuwa ibada zilizopangiwa awali ya mwezi huu zina uhusiano mkubwa na hija, ambayo haifanyiki ko kote Ulimwenguni zaidi ya Makka. Zaidi ya hilo, Waislamu leo po pote walipo Ulimwenguni hushuhudia na kufuatilia ibada ya hija hayi tangu mwanzo

hadi mwisho kupitia vyombo mbali mbali vya habari. Mwenye barua ameutolea uoni huu hoja kadha za kimaandiko na za kiakili, akasisitiza umuhimu wa kuimarisha umoja wa Umma wa Kiislamu kwa kuwaunganisha katika Idil-hajji katika siku moja Ulimwenguni, na akausia kuto kuweka mbele madhehebu na badala yake kutanguliza umoja wa Umma, pia kujali hisia za wafuasi wa madhehebu tafauti wenye uoni uliotajwa.

Kwa kuwa inajibu barua, jawabu hii nayo ilikuwa katika mfumo wa barua, wenye mtiririko wa maandishi bila anuani ya mada wala vichwa vya habari. Aidha haikufafanua kurasa gani katika vitabu vya marejeo ilivotaja yamo yale iliyonukuu, ikitosheka na kutaja jina la kitabu na la mtungaji. Hii ni kwa sababu nakala zilizotegemewa za vitabu hivo ni zile za 'elektroni' zilizomo katika programu za kompyuta, ambazo aghlabu yake hutafautiana na nakala zilizochapwa katika nambari za kurasa.

Juu ya yaliyo tangulia kutajwa ya kiuandishi, na kama ilivo kawaida ya uandishi wa maulama, jawabu hii haikuacha kuwa na mpangilio wa kifikra na mfululizo wa kimawazo, jambo ambalo limewepesisha kwa mfasiri jukumu la kuigawa vifungu vya maudhui na kuviwekea vichwa vya habari muwafaka. Halikadhalika msomaji haitamuwia vigumu kuelewa nukta gani zilijadiliwa na mwenye barua anaposoma majibu yake. Kuepuka ukariri na urudiaji, pamoja na kuchunga heshima ya mwenye barua, hapakuwa na haja ya kunukuu barua yenyewe; la muhimu ni kufahamu kiini cha mjadala katika hoja na jawabu.

Nataraji kwa qudra ya Allah, aliyetakasika na kila upungufu, tafsiri hii ifanikiwe kuufikisha ujumbe uliomo katika maandishi ya asili kwa kadiri inayoweza kufahamika hata kwa watu wa kawaida wasiojaaliwa kuwa na fungu katika fani ya ilmu ya Sharia ya Kiislamu. Kasoro na dosari yo yote katika hilo ni jukumu langu mwenyewe na kinyume na makusudio.

Mfasiri
21 Sha'ban 1431AH
2 / 8 / 2010CE

UTANGULIZI

Shukrani zinamstahikia Mwenyezi Mungu, aliye wawekea waja wake dini iliyo nyooka, iliyo imara jengo lake, madhubuti nguzo zake, dhahiri hoja yake. Na rehma na amani zimshukie Bwana wetu Muhammad, ambaye Mwenyezi Mungu amemhitimishia mitume, na akamjaalia kuwa mbainifu wao kwa kufikisha ujumbe, mkubwa wao kwa dalili, mzito wao kwa hoja, na mbora wao kwa muongozo, pia ziwashukie aali zake na sahaba zake, waliokuwa wakiongoza kwenye haki, na kwa haki wakawa waadilifu, na kila waliowafuatia kwa wema hadi siku ya kufufuliwa.

Baada ya hayo, hakika nimepokea kwa mkono wa shukrani barua yako thamini ya tarekhe 14 Dhul-qa'dah 1430H, nikaitalii na kufahamu madhumuni yake. Zaidi ya shukrani zangu kwako na kadiri ninavyo iheshimu dhati yako tukufu na uoni wako, nilikuwa nasita sita baina ya kutoa maoni yangu juu ya yale yaliyomo baruani humo au kuyanyamazia kimya ili kuulinda uhusiano mzuri na maelewano yaliyopo, pia kuogopea kuzunguka kwenye duara la mijadala. Sikuamua bora kujibu na kuyatolea maoni yale muliyo yataja ila nilipo kuona umekwenda mbali mno ulipo lichukua suala hili kwa jazba za kimadhehebu; nikataka nikubainishie na kila ambaye suala hili limemtatiza kwamba halina uhusiano wo wote na umadhehebu. Bali kauli tuliyo itegemea ndiyo rai ya jumhuri ya Umma wa Kiislamu tangu watangulizi hadi wafuasi, na imekuwa ikifuatwa na wengi wa

viongozi wa Madhehebu Nne, na maulama wao mashuhuri wenye kujumuisha baina ya ilmu ya usuli na ya Qur'ani na Sunna wangali wanaitegemea katika fatwa zao, na wanawaongozea wanaowauliza. Na kwa ajili ya kuepuka jazba ya kimadhehebu sitataja katika jawabu yangu hii isipokuwa maandiko ya maulama wa Madhehebu Nne, ila yale yaliyopokewa kwa masahaba na taabiina na maulama wa miji mikuu wakati wa karne za mwanzo.

Nami kwa kweli kama nimeona ajabu kwa cho chote, basi ajabu yangu iso kikomo ni ile ya kulichukua kwako suala hili kwa jazba ya namna hii; kwasababu naliona hilo lina kishushia hadhi cheo chako cha kitaalamu na kijamii, na sipati katika haya la kukwambia ila neno alilosema Alfaaruuq kwa Abu Ubaida –Allah awaridhie- : "(Afadhali) lau mwengineo angaliyasema hayo...". Ingestahiki mno kwako – pakizingatiwa cheo unachoshika - uwe na hima ya kuyaondosha mawazo haya potofu yanapotoka kwa mtu mwengine. Laiti ningalijua; je hayakuwamo katika hazina ya kielimu - iliyomo kwenye vitabu vya fiqhi, tafsiri na hadithi vilivotungwa na vipawa vya maulama wa Madhehebu Nne, pamoja na waliyoyasema juu ya hili – yale ambayo yanatosha kuwa kizuizi cha tuhuma hii?!

KUWAFIKIANA MASAHABA NA TAABIINA JUU YA KWAMBA KILA NCHI IZINGATIE MUANDAMO WAKE; KHILAFU HAIKUTOKEA ILA BAADA YAO

Inatosha kuanza kwa yale aliyo yasema a'Tirmidhi katika kitabu chake cha "*Sunan*" baada ya kuitaja hadithi ya Kuraibu: "Hadithi ya Ibnu 'Abbaas ni hadithi *sahiih ghariib*[1], na kiutendaji hii ndio hadithi inayofuatwa kwa wenye ilmu, kwamba kila watu wa nchi wana muandamo wao". Kauli yake hii inaonyesha kuwa waliotangulia (wakiwa Sahaba na Taabiina) waliwafikiana juu ya rai hii na khilafu haikutokea ila baadae.

Imamu a'Nawawi katika maelezo yake ya Sahihi Muslim, ameiwekea hadithi hii anuani isemayo: (Mlango wa kubainisha kwamba kila nchi ina muandamo wao na kwamba wakiuona mwezi umeandama katika nchi moja haithibiti hukumu yake kwa nchi zilizo mbali nao). Kisha akasema:

"Kuhusiana na hilo kuna hadithi ya Kuraibu kutoka kwa Ibnu 'Abbaas, nayo inaonyesha wazi yaliyo katika anuani. Na iliyo sahihi kwa maulama wetu ni kwamba kuonekana kwa mwezi nchi fulani hakuwahusu watu wa nchi zote, bali kunawahusu wale tu walio karibu kwa masafa yasiyo punguzwa sala ndani yake. Na kuna kauli ikiwa wakati wa kuchomoza kwa mwezi kwa nchi hiyo ni sawa na wao itawalazimu kufuata. Na kuna kauli ikiwa taifa lao ni moja itawalazimu, vinginevo haiwalazimu. Na baadhi ya watu

[1] Sahihi lakini katika baadhi ya tabaka za sanadi yake imepokewa na mpokezi mmoja tu.

wetu wamesema: kuonekana kwa mwezi sehemu moja kunawahusu watu wote duniani. Na kwa kauli hii tunasema sababu ya Ibnu 'Abbaas kuto kuifuata habari ya Kuraibu ni kwa kuwa habari hiyo ni shahada, na kwa hiyo haithibiti kwa mtu mmoja; lakini dhahiri ya hadithi yake ni kuwa yeye hakukataa kuifuata kwa sababu hii, bali alikataa kwasababu tu kuonekana mwezi huko hakuthibiti hukumu yake kwa walio mbali."

Ibnu 'Abdil-Barr kasema katika "*a'Tamhiid*":

"Maulama wamekhitalifiana katika hukumu wakiuona mwezi watu wa nchi moja pasina nchi nyengine. Imepokewa kwa Ibnu Abbaas na Ikrima na al Qasim bin Muhammad na Salim bin Abdalla kuwa wamesema kila watu wa nchi na muandamo wao, nayo ndiyo kauli ya Is'haaq bin Raahawaihi. Hoja ya wenye kauli hii ni hadithi aliyotuhadithia Abdalla bin Muhammad bin Abdil-Muumin, kasema ametuhadithia Muhammad bin Bakri bin Daasa, kasema ametuhadithia Abu Daud, kasema ametuhadithia Musa bin Ismail, kasema ametuhadithia Ismail bin Ja'far, kasema amenipa habari Muhammad bin Abi Harmala, kasema amenipa habari Kuraibu kwamba Ummu al Fadhli bint al Haarith alimtuma kwa Muawiya huko Sham, kasema nikenda Sham nikamtimizia haja yake ukaniandamia mwezi niko Sham, tukauona mwezi mwandamo usiku wa kuamkia Ijumaa, kisha nikaja mwisho wa mwezi, akaniuliza Ibnu Abbaas kisha akaulizia mwezi akasema: Lini mliuona mwezi? Kasema: Nikasema iliuona

usiku wa kuamkia Ijumaa. Akasema: Wewe uliuona? Nikasema: Naam, na watu waliuona na wakafunga, na Muawiya kafunga. Akasema: Lakini sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi na kwa hiyo tutaendelea kufunga mpaka tukamilishe siku thalathini au tuuone. Nikasema: Na hutosheki na kuona kwa Muawiya? Akasema: La, hivi ndivo alivotuamuru Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie."(mwsh)

Na kasema katika *al Istidhkaar*:

"Watu wa Madina wamepokea kwa Malik, nayo ndiyo kauli ya al Mughira na Ibnu Diinar na Ibnu al Maajishuun kwamba kuonekana mwezi hakuwalazimu isipokuwa watu wa nchi ambamo umeonekana ila kama Mtawala wa nchi hizo atawajumuisha watu wote katika muandamo huo."(mwsh)

Na al Maaruudi kasema katika "*al Haawi*":

"Kama wameuona watu wa nchi na hawakuuona watu wa nchi nyengine mwezi wa Ramadhani, basi as'habu zetu wamekhitalifiana kuhusu watu wa nchi ile ambayo hawakuuona katika rai tatu:"

"Rai ya kwanza: Ni juu yao wafunge kwani kuuona watu wote si sharti katika kuwajibika funga, na fardhi ya Mwenyezi Mungu juu ya wote ni moja."

"Rai ya pili: Haiwalazimu kufunga mpaka wauone; kwasababu nyota na sayari zinazo chomoza na kuzama zinaweza zikatafautiana wakati ikiwa nchi ni tafauti, na kila watu wameamrishwa kwa mujibu wa wakati wao wa

kuchomoza na kuzama. Unaona kuwa alfajiri inaweza ikatangulia kuchomoza katika nchi fulani kabla nchi nyengine; halikadhalika jua linaweza likazama nchi fulani kabla nyengine, kisha mfungaji akawa anazingatia kuchomoza kwa alfajiri na kuzama kwa jua katika nchi yake, basi ni vivyo hivyo mwezi muandamo."

"Rai ya tatu: Wakiwa katika ukanda mmoja itawalazimu wafunge, na wakiwa katika kanda mbili tafauti haitawalazimu; kwani imepokewa kwamba Thawban alikwenda Madina kutoka Sham akawapa habari ya kuonekana mwezi kabla Madina kwa siku moja, akasema Ibnu Abbaas, "Hautulazimu, wao wana Sham yao na sisi Hijaz yetu", akaipa Hijaz hukumu moja ingawa mna nchi tafauti, na akatafautisha baina yake na Sham." (mwsh)

Na Ibnu Hajar al Haitami kasema katika "*al Fatawa al Fiqhiyya al Kubra*":

"Ama aliyo yataja Mufti aliyetajwa katika kujibu kauli ya mwenye kuuliza ukionekana mwezi Makka na haukuonekana katika ardhi ya Bajila[1], hayo ni sahihi. Kilicho thibiti katika hilo ni kwamba linalo zingatiwa ni kuungana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi au kutafautiana katika hilo (baina ya nchi), siyo masafa ya kupunguza sala katika safari. Kasema kwenye "*al Anwaar*", na linalo kusudiwa kwa kutafautiana kwa wakati wa kuchomozewa na mwezi ni kuwepo umbali baina ya nchi

[1] Iko mashariki ya Makka.

mbili kiasi cha kwamba lau ukionekana mwezi katika moja wapo, aghlabu hauonekani katika nyengine."

Sheikh Taju'din a'Tibrizi kasema:

"Kuonekana kwa mwezi katika nchi mojawapo kunawajibisha ithibiti hukumu yake mpaka umbali wa farsakhi ishirini na nne, kwasababu katika masafa yaliyo chini ya hapo nchi hazitafautiani. Kasema a'Subki na al Isnawi: Zinaweza zikatafautiana na ikawa kuonekana mwezi katika nchi moja wapo kunalazimisha uonekane katika nyengine bila kinyume cha hayo; kwani usiku unaingia katika nchi za mashariki kabla kuingia katika zile za magharibi, na kwa hiyo zinapo tafautiana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi inalazimika ukionekana mwezi katika nchi ya mashariki uonekane katika nchi ya magharibi bila kinyume; ama zinapo ungana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi inalazimika ukionekana katika moja wapo ya nchi mbili hizo uonekane katika ya pili."(mwsh)

Imekuja pia katika "*al Fatawa al Fiqhiyya al Kubra*":

"Na aliulizwa –Allah anufaishe kwaye- kuhusu kuonekana kwa mwezi tukisema ukaribu na umbali ni kwa kutafautiana na kuungana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi, je inalazimika kutokana na hilo ionekane tafauti baina ya watu wa nchi za mashariki na magharibi mwanzoni mwa mwezi na mwishoni, wakati haikuwa mashuhuri kwa watu wa nchi nyenginezo ila kuwafikiana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi; nini sababu ya hilo; je ni kuwa tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi haionekani katika sehemu wanazoishi watu kwa wingi au sivyo? Ukisema

ni la mwanzo basi ni wa nini mzozo uliopo baina ya maimamu katika kuupa uzito mtafautiano wa wakati wa kuchomozewa na mwezi na muungano wa hilo na masafa ya kupunguza sala kwa safari? Akajibu kwa kusema, 'Ndiyo inalazimika kutokana na hilo (yaani mtafautiano na muungano wa wakati wa kuchomozewa na mwezi) hayo (ya kuonekana tafauti baina ya watu wa nchi za mashariki na magharibi mwanzoni na mwishoni mwa mwezi), kwani al Subki na al Isnawi wamesema wazi kwamba wakati wa kuchomozewa na mwezi ukitafautiana inaweza ikalazimika kutokana na kuonekana mwezi katika nchi mojawapo uonekane katika nyengine bila ya kinyume chake, kwani usiku unaingia katika nchi za mashariki kabla kuingia katika zile za magharibi, na kwa hiyo zinapo tafautiana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi inalazimika ukionekana mwezi katika nchi ya mashariki uonekane katika nchi ya magharibi bila kinyume; ama zinapo ungana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi inalazimika ukionekana katika nchi mojawapo uonekane katika nyengine'."(mwsh)

Na kwenye *'al Minhaj'* na sherehe yake *'Tuhfat al Muhtaj'*, na maelezo ya al Sharwani na Ibnu Qasim al Abbaadi, yamo yanayo tilia nguvu haya yaliyo tangulia.

NCHI ZILIZO KARIBIANA KUWA NA MUANDAMO MMOJA KWA KUWA WAKATI WAO WA KUCHOMOZEWA NA MWEZI NI MMOJA

Al Shiirazi kasema kwenye "*al Muhadh-dhab*":

"Na wakiuona mwezi katika nchi moja na hawakuuona katika nchi nyengine basi zikiwa ni nchi mbili zilizo karibiana watawajibikiwa watu wa nchi mbili hizo kufunga; na zikiwa ziko mbali mbali haziku karibiana watawajibikiwa kufunga nchi waliouona pasina nchi wasio uona, kwa dalili ya mapokezi ya Kuraibu, kasema: 'Nilikwenda Sham nikauona mwezi muandamo usiku wa kuamkia Ijumaa, kisha nikaja Madina akaniuliza Abdalla bin Abbaas lini mliuona mwezi? Nikasema usiku wa kuamkia Ijumaa. Akasema wewe uliuona? Nikasema ndiyo na watu waliuona na wakafunga, na Muawiya akafunga. Akasema lakini sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi na kwa hiyo tutaendelea kufunga mpaka tukamilishe idadi ya siku (thalathini) au tuuone. Nikasema je hutosheki na kuuona kwa Muawiya? Akasema hivi ndivo alivo tuamrisha Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie'."(mwsh)

Na a'Nawawi kasema katika sherehe yake "*al Majmuu*":

"Suala la Tatu: Wakiuona mwezi wa Ramadhani katika nchi moja na hawakuuona katika nchi nyengine, basi zikikaribiana nchi mbili hizo hukumu yao ni sawa na hukumu ya nchi moja, na inawalazimu watu wa nchi ya pili wafunge bila khilafu (baina ya wenye ilmu). Zikiwa nchi mbili hizo moja iko mbali na nyengine kuna kauli mbili mashuhuri katika njia mbili:"

"(Iliyo sahihi zaidi): Hakuwajibiki kufunga kwa watu wa nchi ya pili, na hii ndiyo kauli aliyo iyakinisha Msanifu na Sheikh Abu Hamid na al Bandaniji na wengineo, na kaisahihisha al Abdari na a'Raafii na walio wengi."

"(Kauli ya pili): Inawajibika [kufunga kwa watu wa nchi ya pili], na hii ndio kauli a'Simyariy na kaisahihisha al Qadhi Abu a'Tayyib na a'Daarami na Abu Ali a'Sinjiy na wengineo. Wamejibu hawa kuhusu hadithi ya Kuraibu kutoka kwa Ibnu Abbaas kwamba yeye (Ibnu Abbaas) haikumthibitikia kuonekana kwa mwezi katika nchi nyengine kwa ushahidi wa waadilifu wawili. Lakini kauli sahihi ni ya mwanzo."

"Kuhusu namna ya kuzingatia umbali na ukaribu baina ya nchi kuna kauli tatu:

"(Iliyo sahihi zaidi): Nayo ndiyo waliyo iyakinisha jumhuri ya maulama wa Iraqi na a'Saidalani na wengineo kwamba umbali wa baina ya nchi unatafautiana kwa tafauti za wakati wa kuchomoza kwa mwezi kama ilivo Hijazi, Iraqi na Khurasani; na ukaribiano ni kuto kuwapo tafauti kama ilivo Baghdadi na al Kufa, na a'Rayyu na Qazwini, kwasababu wakati wa kuchomoza mwezi kwa hawa ni sawa na wakati wa hawa, kwa hiyo wakiuona hawa huwa kuto kuuona kwa wenzao ni kwa sababu ya wao kuto kufanya hima katika kuuangalia au kwa sababu ya kuwepo kizuizi; kinyume na wanaotafautiana wakati wa kuchomoza kwa mwezi."

"(Ya pili): Ni kuzingatia umoja wa ukanda ziliomo nchi au kutafautiana ukanda ziliomo; ukiwa ukanda ni

mmoja nchi hizo huwa zimekaribiana, vinginevo huwa ziko mbali mbali, na hii ndiyo kauli ya a'Simyariy na wengineo."

"(Ya tatu): Kwamba umbali wa nchi na nchi ni masafa ya kupunguza sala, na ukaribiano ni chini ya masafa hayo; na hii ndiyo kauli ya al Faurani na Imamu al Haramaini na al Ghazali na al Baghawi na wengineo miongoni mwa Wakhurasani. Imamu al Haramaini kadai kuwa kuna maafikiano juu ya kauli hiyo kwasababu kutafautiana wakati wa kuchomoza kwa mwezi kunahitajisha kujua hisabu na kuwahukumisha wenye ilmu ya nyota wakati misingi ya Sharia haikubali hilo, na kwa hiyo inawajibika kuzingatia masafa ya kupunguza sala, ambayo Sharia imeyafungamanisha na nyingi kati ya hukumu za kisharia. Na hii ni dhaifu kwasababu jambo la kuandama kwa mwezi halihusiani na masafa ya kupunguza sala. Hivyo, kauli sahihi ni kuzingatia wakati wa kuchomoza kwa mwezi kama ilivotangulia. Kwa msingi huu kama patakuwa na shaka katika kuwafikiana wakati wa kuchomoza kwa mwezi haitawalazimu wale ambao hawakuuona mwezi kufunga kwasababu hali ya asili ni kuto kuwajibika kufunga, na kwasababu kufunga huwajibika kwa kuuona mwezi kutokana na hadithi, na kuuona hakujathibiti kwa hawa kutokana na kuto kuthibiti ukaribu wao kutoka nchi iliyo uona mwezi. Kauli hii niliyoitaja ndiyo mashuhuri kwa maulama wetu katika njia mbili, lakini al Maarudiy na a'Sarkhasiy peke yao wamechukua njia mbili nyengine; ambapo al Maarudiy kasema wakiuona katika nchi moja pasina nchi nyengine kuna kauli tatu:"

"(Ya kwanza): Inawalazimu kufunga wale ambao hawakuuona kwasababu fardhi ya Ramadhani haitafautiani kwa tafauti za nchi na Ramadhani imeshathibiti."

"(Ya pili): Haiwalazimu kwasababu kuchomoza na kuzama kwa jua, mwezi, n.k. kunaweza kukatafautiana kwa kutafautiana nchi, na watu wa kila nchi wamesemezwa kwa mujibu wa wakati wao wa kuchomoza na kuzama kwa jua na mwezi; huoni alfajiri inaweza ikatangulia kuchomoza katika nchi moja na ikachelewa katika nchi nyengine, na halikadhalika jua linaweza likaharakiza kuzama katika nchi moja na likachelewa katika nchi nyengine, kisha kila nchi inazingatiwa kuchomoza alfajiri yake na kuzama jua lake kwa wakaazi wake, basi halikadhalika mwezi."

"(Ya tatu): Zikiwa nchi mbili zimo katika ukanda mmoja itawalazimu, vinginevo hawalazimu. Haya ndiyo maneno ya al Maarudiy."

"A'Sarkhasiy kasema wakiuona watu wa upande fulani pasina upande mwengine basi yakiwa masafa ni karibu baina yao itawalazimu wote kufunga; na kipimo cha ukaribu iwe aghlabu wakiuona hawa haufichikani kwa wale ila kwa sababu ya kizuizi, sawa katika hilo ikiwa ni masafa ya kupunguza sala au mengineyo. Kasema yakiwa masafa ni mbali baina yao kuna kauli tatu:"

"(Ya kwanza): Inawalazimu wote, na ndiyo aliyochagua Abu Ali a'Sinjiy."

"(Ya pili): Haiwalazimu."

"(Ya tatu): Yakiwa masafa baina yao ni kadiri ya kwamba haifikiriwi uonekane kwa hawa na ufichikane kwa

wale bila kuwepo kizuizi itawalazimu wote, na yakiwa masafa kadiri ya kwamba inafikiriwa kufichikana kwa wale haitawalazimu."

"* Kwa hiyo katika suala hili kumekuwa na kauli sita:

Ya kwanza: Itawalazimu watu wote Duniani ukionekana po pote Duniani.

Ya pili: Itawalazimu watu walio ukanda wa nchi iliyo uona pasina wengine.

Ya tatu: Itawalazimu kila nchi inayowafikiana na nchi iliyo uona katika wakati wa kuchomoza mwezi pasina nchi nyengine, na hii ndiyo kauli iliyo sahihi kuliko nyenginezo.

Ya nne: Itawalazimu kila nchi ambayo haifikiriwi kuwa utafichikana kwao bila kuwepo kizuizi pasina nchi za wengine, nayo ni katika aliyonukuu a'Sarkhasiy.

Ya tano: Itawalazimu walio chini ya masafa ya kupunguza sala pasina wengine.

Ya sita: Haiwalazimu ila nchi iliyo uona mwezi, nayo ni katika aliyonukuu al Maarudiy, na Allah anajua zaidi."(mwsh)

Abu Al-Abbaas al Qurtubiy kasema katika "*al Muf-him*":

"Na kauli ya Ibnu Abbaas: ((na kwa hiyo tataendelea kufunga mpaka tukamilishe thalathini au tuuone)), kisha kasema mwisho wake: ((hivi ndivo alivotuamuru Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie)); ni neno la wazi la kuyanasibisha hayo kwa Mtume –rehma za Allah na

amani zimshukie- na kwamba yeye kaamuru hivo. Hiyo ni hoja ya kwamba nchi zikiwa zimetengana mbali kama zilivotengana Sham na Hijazi au karibu ya hivo, linalowajibika kwa watu wa kila nchi ni kufuata uonaji wao wa mwezi na siyo uonaji wa nchi nyengine, hata ukiwa umethibiti kwa Imamu Mkuu anayetawala nchi hizo zote, madamu hajawalazimisha watu kufuata huko, kwani haijuzu kumpinga; kwasababu suala hili ni la kiijtihadi lenye khilafu ndani yake, lakini hakubaki ijtihadi Imamu akitowa hukumu, wala si halali kumpinga. Huoni kuwa Muawiya – Amir al Muuminiina – alifunga kwa kuonekana mwezi na watu wakafunga kwa kuonekana mwezi huko Sham, kisha Ibnu Abbaas hakuzingatia hayo, bali alibaki katika hukumu ya kuonekana mwezi nchini mwake yeye. Sababu ya kufanya hivo wanaijua wenye ilmu ya nyota; kwani inabainika katika ilmu hiyo: kwamba minyanyuko ya kanda mbali mbali inakhitalifiana, na kwa hiyo wakati wa kuchomoza kwa mwezi na kuzama unakhitalifiana, ambapo mwezi unachomoza na kuzama kwa watu wa nchi fulani kabla kuchomoza na kuzama kwa watu wa nchi nyengine. Na kwa msingi huu: haidhihiri taathira ya hili isipokuwa baina ya nchi zilizotengana mbali sana, na siyo baina ya ambazo zimekaribiana, na Mwenyezi Mungu anajua zaidi."

"Hii ndiyo rai ya Ibnu Abbaas, Salim, al Qasim, na Ikrima. Nayo ndiyo kauli ya Is'haq, na ndiyo aliyo ionesha a'Tirmidhi alipoweka mlango wa: 'Watu wa kila nchi wana muandamo wao'. Na Abu Amr bin Abdulbarri amenakili Ijmai (maafikiano ya wenye ilmu) juu ya kwamba kuonekana

mwezi nchi moja hakuzingatiwi katika nchi zilizo mbali kama al Andalus kutoka Khurasan[1], akasema, 'Na kila nchi ina uonaje wake wa mwezi, ila zile ambazo zitakuwa kama mji mmoja mkubwa, na zile ambazo pande zake zinakaribiana kati ya nchi za Waislamu'."

"Nimesema –msemaji ni Abu al Abbaas al Qurtubi-: Na ijmai hii aliyo isimulia Abu Amr inaonesha kuwa khilafu iliyopo katika suala hili ni kuhusu nchi zilizo karibiana tu, na hakutaja ndani yake hukumu ya taifa moja, na sisi tataitaja insha Allah Taala."

"Ibnu al Mundhir kasema: 'Kumekuwapo khilafu katika mwezi wakiuona watu wa nchi moja na hawakuuona wa nchi nyengine: Kuna waliosema: Watu wa kila nchi wana muandamo wao.' Na akawataja wale ambao wengi wao wametangulia kutajwa."

"Na wengine wamesema: Ikithibiti kuwa watu wa nchi fulani wameuona itakuwa ni juu yao kulipa siku wasizofunga. Nayo ndiyo kauli ya al Laith, a'Shaafi' na Ahmad, na siijui ila ndio kauli ya al Muzni na al Kufi."

Kisha akasema baada ya kutaja khilafu hiyo baina ya maulama katika kuziunganisha nchi na nyengine katika hukumu:

"Na iliyo sahihi ni kutafautika –yaani baina ya nchi zilizokaribiana na zilizotengana-; kwa dalili ya ijmai aliyo isimulia Abu Amr, na kwa hiyo unachukuliwa ujumla wa maneno ya Mashekhe kuwa unakusudia nchi zilizokaribiana, na Mwenyezi Mungu anajua zaidi." (mwsh)

[1] Al Andalus sasa ni Spain, na Khurasan ni Iran.

NCHI ZA MASHARIKI KUTAFAUTIANA NA ZA MAGHARIBI KATIKA WAKATI WA KUCHOMOZA NA KUZAMA KWA JUA NA MWEZI

Al Qarrafi kasema katika "*al Dhakhiira*":

"Mwenyezi Mungu ameweka nyakati ziwe sababu za hukumu za kisharia, kama kuchomoza alfajiri, kupindukia jua, na kuonekana mwezi, kama alivoweka vitendo viwe sababu za hukumu za kisharia, mfano kuiba na kuzini. Na nyakati zinatafautiana kwa mujibu wa nchi, kwani hauwi upindukiaji wa jua kwa watu fulani ila huwa ni alfajiri kwa watu wengine, na magharibi kwa wengine, na nusu ya usiku kwa wengine. Bali kila linapotembea jua daraja moja basi daraja hiyo hiyo ni alfajiri, kuchomoza jua, kuchwa jua, nusu ya usiku, nusu ya mchana, na majina yote mengineyo ya wakati hunasibishwa kwa daraja hiyo hiyo kwa mujibu wa nchi tafauti. Na Mwenyezi Mungu amewaamuru kila watu kwa yale yanayofanyika kwenye nchi yao siyo kwenye nchi ya wengine, hakuamuriwa mtu kufuata upindukiaji jua wa nchi nyengine wala alfajiri ya nchi hiyo, na hili limewafikiwa kwa ijmai (makubaliano) ya wote. Vile vile mwezi nyakati zake za kuchomoza zinatafautiana; unaonekana nchi za magharibi wakati hauonekani nchi za mashariki ila katika usiku wa pili kwa mujibu unavojificha katika muale wa jua. Hili linajulikana bila tabu kwa mwenye kuliangalia. Na kwa kawaida kila mtu anapaswa afuate uonaji mwezi wa nchi yake na isimlazimu hukumu ya uonaji wa nchi nyengine hata kama umethibiti kwa njia zisizo shaka, kama ambavyo haitulazimu sala ya alfajiri hata tukiwa tuna hakika kuwa

alfajiri imeshachomoza kwa wale walio mashariki ya nchi yetu kama alivosema. Hili ndilo alilo ashiria al Bukhari katika hadithi hii aliposema kwamba watu wa kila nchi wana muandamo wao, ingawa hilo halikupokewa kutoka kwa Umar bin al Khattaab wala mwengine kati ya makhalifa kwamba alikuwa akiwaandikia barua nchi mbali mbali na kutuma mjumbe kwamba mimi nimeuona mwezi basi fungeni, bali walikuwa wakiwaacha watu na mwezi wao walio uona, na kwa hiyo inakuwa ni sharti lilowafikiwa na wote."(mwsh)

Na kasema katika "*al Furuuq*": "Ukweli ni kwamba unazingatiwa kwa kila nchi uonaji wao na muandamo wao kama inavozingatiwa kwa kila nchi alfajiri yao na adhuhuri yao."

Kasema pia:

"Ikithibiti makubaliano juu ya kwamba nyakati za sala zinatafautiana kwa kutafautiana nchi zilizo mbali mbali, na kwamba kila nchi wana alfajiri yao na adhuhuri yao na nyenginezo katika nyakati, basi inalazimika kuwe na tafauti hiyo katika miandamo ya mwezi; kwasababu katika nchi za mashariki ukiwa mwezi katika muale wa jua, na likawa jua linashuka pamoja na mwezi upande wa magharibi, basi jua halifiki kwenye upeo wa magharibi ila na mwezi unakuwa umeshatoka kwenye muale wa jua na kwa hiyo watauona watu wa magharibi pasina kuuona watu wa mashariki. Hii ni mojawapo ya sababu za kutafautika kuonekana kwa mwezi, na kuna sababu nyenginezo zimetajwa katika elimu ya nyota haipendezi kuzitaja hapa; niliyotaja ni yale tu yaliyo mepesi kufahamika. Ikiwa uonaji wa mwezi unatafautika kwa

kutafautika nchi zilizo mbali mbali, itawajibika iwe kila nchi wana wakati wao wa kuuona mwezi kama kwamba kila nchi wana alfajiri yao na nyenginezo katika nyakati za sala; hii ni haki iliyo wazi na ni sahihi pasina nyengine. Ama kuwajibika saumu juu ya kanda zote kwa kuonekana mwezi katika nchi mojawapo kati yake, hili liko mbali na misingi, na dalili hazikuonesha hivo, basi ulijue."

Na kasema Abu Abdalla al Qurtubi mwenye tafsiri:

"Na wamekhitalifiana anapotoa habari mtu ya nchi fulani kuuona mwezi, kwani ima nchi hiyo itakuwa karibu au mbali; ikiwa karibu basi hukumu ya mwezi ni moja, na ikiwa mbali basi watu wa kila nchi wana uonaji wao wa mwezi. Kauli hii imepokewa kwa Ikrima, na Al Qaasim, na Salim, na imepokewa kwa Ibnu Abbaas, na ndiyo kauli ya Is'haaq, na ndiyo aliyo iashiria Al Bukhari alipoweka mlango wenye anuani: Watu wa kila nchi wana uonaji wao wa mwezi". (mwsh)

Na Ibnu Al Arabi kasema katika "*Ahkaamu Al Qur'aan*":

"Kumekuwa na khilafu katika kuufahamu undani wa kauli ya Ibnu Abbaas hii: kuna usemi aliikataa (habari ya Kuraib) kwasababu ni habari ya mtu mmoja. Na kuna usemi aliikataa kwasababu nchi hizo zinatafautiana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi, na hii ndiyo sahihi, kwasababu Kuraib hakushuhudia bali alitoa habari ya hukumu iliyothibiti kwa kushuhudiwa, na hakuna khilafu katika kwamba hukumu iliyothibiti kwa kushuhudiwa inatosheleza kutolewa kwa habari ya mmoja. Mfano wake ni kama

ingethibiti kwamba umeandama usiku wa kuamkia Ijumaa huko Aghamaat na umeandama huko Ishbiilia usiku wa kuamkia Jumamosi ambapo huwa watu wa kila nchi wana muandamo wao kwasababu (nyota ya) Suhail inaonekana kutoka Aghamaat wakati haionekani kutoka Ishbiilia, na hili linaonesha kutafautiana kwa wakati wa kuchomozewa na mwezi ". (mwsh)

Na Ibnu Rushd kasema katika "*Bidaayat al Mujtahid wa Nihaayat al Muqtasid*":

"Na tukisema kuwa kuonekana mwezi kunathibiti kwa kupewa habari kwa yule ambaye hakuuona, je hilo linavuka nchi hadi nchi nyengine? Namaanisha je wanawajibikiwa watu wa nchi fulani wasipouona mwezi wafuate katika hilo uonaji wa nchi nyengine ama kila nchi ina uonaji wake? Hapo kuna khilafu. Ama Malik wamepokea kwake Ibnu Al Qaasim na watu wa Misri kwamba ikithibiti kwa watu wa nchi moja kuwa watu wa nchi nyengine wameuona mwezi basi ni juu yao kuilipa ile siku wasiyofunga ambayo wengine waliifunga, na hii ndiyo kauli ya a'Shaafi'i na Ahmad."

"Na watu wa Madina wamepokea kwa Malik kwamba uonekano wa mwezi hauthibiti kwa kupewa habari kwa wasio wa nchi ambayo umeonekana ila akiwa imamu mtawala anawaamuru watu hivyo, na hii ndiyo kauli ya Ibnu al Maajishuun na al Mughiira kati ya as'haab zake Malik."

"Na wamekubaliana wote kuwa hilo halizingatiwi katika nchi mbili zilizo mbali kama al Andalus na al Hijaaz."

"Sababu ya khilafu hii ni upingano wa mapokeo na mazingatio. Mazingatio ni kwamba nchi zikiwa nyakati zake

za kuchomoza mwezi hazikutafautiana tafauti kamili inawajibika zipewe hukumu moja kwasababu nchi hizo huwa kama zenye upeo mmoja; na zikitafautiana tafauti kubwa haiwajibiki zipewe hukumu moja."

"Ama mapokeo ni yale aliyo yapokea Muslim kutoka kwa Kuraibu kwamba Ummu al Fadhli bint al Haarith alimtuma kwa Muawiya huko Sham, kasema nikenda Sham nikamtimizia haja yake na ukaniandamia mwezi nami niko Sham, nikauona mwezi mwandamo usiku wa kuamkia Ijumaa, kisha nikaja Madina mwisho wa mwezi, akaniuliza Abdalla bin Abbaas kisha akaulizia mwezi akasema: Lini mliuona mwezi? Nikasema niliuona usiku wa kuamkia Ijumaa. Akasema: Wewe uliuona? Nikasema: Naam, na watu waliuona na wakafunga, na Muawiya kafunga. Akasema: Lakini sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi na kwa hiyo tutaendelea kufunga mpaka tukamilishe siku thalathini au tuuone. Nikasema: Je hutosheki na kuona kwa Muawiya? Akasema: La, hivi ndivo alivotuamuru Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie."

"Dhahiri ya mapokeo haya inamaanisha kwamba kila nchi ina uonaji wake wa mwezi, iwe karibu au mbali. Na mazingatio yanatafautisha baina ya nchi zilizo mbali na zilizo karibu, na hususan zile ambazo umbali wake katika longitudo na latitudo ni mkubwa".

Ibnu Abdu'Razzaaq kasema katika "*al 'Adhbu a'Zulaal*":

"Bali hadithi za kuona mwezi zote zinaonesha hilo – yaani kuzingatia tafauti za wakati wa kuchomozewa na mwezi- na hususan hadithi ya Kuraibu kama ulivojua. Vile

vile yanayoshuhudiwa na kuzingatiwa; kwani uonekano wa mwezi unaotokea jioni baada ya mwezi kuwa pamoja na jua kisha kutoka katika muale wa jua, jambo ambalo linazingatiwa katika kuainisha mwanzo wa saumu na mwisho wake kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume na Ijmai, uonekano huo wa mwezi hapana shaka kuwa unatafautiana (baina ya nchi) zinapo tafautiana peo."

Kasema pia:

"Na kwa hayo tiliyotaja miongoni mwa maneno ya al Baaji na Ibnu Abdil'Hakam na Ibnu Abdil'Barri na al Qurtubi linabainika kosa la mwenye kumnasibishia Malik na as'haabu zake kauli ya kuenea hukumu ya kuonekana mwezi nchi zote hata pamoja na kuwa ni mbali sana, na hali wao wamewafikiana wote juu ya kwamba hakuna kupelekeana habari pakiwa ni mbali sana, bali haijuzu wala hailazimiki kufanya hivo iwapo inawezekana kuuona watu wa nchi fulani na kuto kuuona wengine kama alivosema Ibnu Abdil'Hakam. Hayo ni kwasababu uonekano unaozingatiwa kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna na Ijmai ni uonekano unaotokea jioni baada ya mwezi kuwa pamoja na jua kisha kutoka kwenye muale wa jua, kama ulivojua, unaweza kuwa wazi wazi katika baadhi ya peo na usiwezekane siku hiyo hiyo katika peo nyengine. Hilo ni kwa kushuhudiwa na kwa hisabu za kifalaki za uhakika zinazotokana na uangalizi wa kitaalamu na kushuhudiwa katika miaka mingi." (mwsh)

Kasema pia:

"Kutokana na hayo, mwenye kusema kuwa uonekano wa mwezi wa nchi moja unazilazimu nchi zote hata pamoja na umbali sana, huyo amepinga mapokeo na mazingatio ya akili, kwani mapokeo na mazingatio ya akili yanakubaliana kuwa hapana kupelekeana habari pakiwa na umbali mkubwa ambao inawezekana wakauona mwezi watu wa nchi moja na wasiuone wa nchi nyengine."

"Aidha, vipi ziwe sawa nchi zote kwa hali yoyote katika kuuona mwezi wakati tumeshasema kuwa ijmai imepita juu ya kwamba uonekano wa mwezi unaokusudiwa ambao Sharia imeuainishia mwanzo wa saumu na mwisho wake ni ule uonekano unaotokea jioni baada ya mwezi kuwa pamoja na jua kisha kutoka kwenye muale wa jua, na kwamba ni katika yasiyo na shaka kuwa uonekano wa mwezi baada ya kuzama jua unaweza kuwa wazi wazi katika baadhi ya peo na usiwezekane katika peo nyengine kwa mujibu wa kutafautiana katika umbali wa longitudo au latitudo au wa namna zote mbili."

Kasema pia:

"Kisha kauli yake –rehma za Allah na amani zimshukie: 'Fungeni kwa kuuona na fungueni kwa kuuona' imefasiriwa kwa hadithi nyengine ambayo ni: 'Mkiuona mwezi fungeni na mkiuona fungueni', kwasababu maana ya 'Fungeni mkiuona' yaani fungeni kwa kuuona kwenu mwezi, kwa dalili ya 'Mkiuona mwezi fungeni...' na kwa hiyo amri iliyomo katika hadithi zote mbili imeelekezwa kwa kila pote la waislamu na hapana tatizo, wala hakuna katika hilo ishara

hata ndogo inayoashiria kuwa kuuona kwa baadhi ya nchi kunawaenea watu wote ulimwenguni."

Kisha kasema:

"Aidha, kauli yake -rehma za Allah na amani zimshukie: 'Fungeni kwa kuuona...' ndiyo kama kauli Yake Taala:

((وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّى يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ))

{**Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku**} Albaqara: 187, kwani amri iliyomo katika aya hii na hadithi hiyo imeelekezwa kwa umma wote na hapana tatizo, lakini kwa kuwa umeainishwa katika aya hii mwanzo wa kujizuia kula na mwisho wake kwa kuchomoza alfajiri na kuchwa kwa jua, wakati katika hadithi umeainishwa mwanzo wa saumu na mwisho wake kwa kuuona mwezi baada ya kuzama kwa jua; na yote hayo ni katika yanayotafautiana kwa kutafautiana peo, bila shaka. Na kwa hiyo hapana budi kuzingatia alfajiri ya kila nchi na magharibi ya kila nchi baada ya kuzama jua, wala hapana tafauti baina ya hayo yote. Mwenye kudai kuna tafauti ni juu yake kuleta dalili inayokubalika kisharia, kifalaki na kiakili. Kisha haya yote ni kama tutachukulia kuwa Mtume -rehma za Allah na amani zimshukie- hakusema zaidi ya kauli yake: 'Fungeni kwa kuuona na fungueni kwa kuuona', ama kwa vile ameongeza: 'Na iwapo utafichikana msiuone kamilisheni idadi siku thalathini' na katika riwaya nyengine 'Na yakikuzuilieni mawingu kuuona kamilisheni idadi siku thalathini', basi haina maana kuichukulia hadithi kwa maana ya kueneza hukumu moja kwa nchi zote bila masharti. Bali kauli yake –rehma za Allah na amani

zimshukie: 'Yakikuzuilieni mawingu kuuona' ni katika yanayo onesha kuwa watu wa kila nchi wanaamrishwa wafuate hali waliyo nayo bila kutafautisha baina ya masafa ya mbali na mengineyo. Hayo ni kwasababu tamko hili linatuamrisha kukamilisha idadi ya siku thalathini iwapo mawingu yatatuzuia kuuona mwezi, jambo ambalo ni sawa iwapo haujaonekana duniani kote na iwapo umeonekana nchi ya mbali na iwapo umeonekana nchi ya karibu. Na kwa kuwa tamko hili ni sawa katika sura hizo tatu, vipi itasihi kuichukulia kauli yake –rehma za Allah na amani zimshukie: 'Fungeni kwa kuuona na fungueni kwa kuuona' kwa maana ya kujumuisha watu wote ulimwenguni bila masharti? Bali kufanya hivo ni katika kufuata mwanzo wa hadithi -tukijaalia unajumuisha watu wote- na kuto kushughulika na mwisho wa hadithi ingawa maneno yaliyokusudiwa hasa yamo mwishoni humo."

Halafu akasema:

"Aidha, kwa kuwa mleta sharia ameacha tamko la wazi la kujumuisha watu wote ulimwenguni katika kuuona mwezi akatumia badala yake tamko hili linalokusanya sura tatu hizo, basi hiyo ni dalili ya kwamba kuonekana mwezi mahala pamoja hakujumuishi hukumu yake watu wote duniani; kwani kama ingalikuwa kunajumuisha watu wote duniani angalitumia tamko la wazi kumaanisha hilo, ambalo ni 'Fungeni kwa kuonekana mwezi popote na fungueni kwa kuonekana mwezi popote; ikiwa hamkuuona kabisa ...', kwasababu yeye hakutumwa isipokuwa ili awabainishie watu walichoteremshiwa; na si katika kubainisha linapoachwa

tamko la wazi katika kumaanisha hukumu likatumiwa tamko jengine. Aidha, kujumuisha watu wote katika hadithi hiyo kunahitaji pawe na makadirio ya maneno yasiyokuwamo katika hadithi, nayo ni 'kwa kuonekana popote' au 'hata ukionekana sehemu moja (duniani)' wakati asili ya maneno ni kutokuwapo makadirio hayo."

Kasema aidha:

"Juu ya hivo, hadithi za kuuona mwezi zimekuja kwa matamko tafauti na yote yanamaanisha kuwa kila pote la Waislamu litegemee yale litakayo yashuhudia ikiwa ni kuuona mwezi au kuzingwa na mawingu."(mwsh)

Kisha akataja idadi kadha ya hadithi hizo.

Kuna maandiko mengineyo ya wengi kati ya maulama wa kimaaliki yanatilia nguvu maana hii na kubainisha kwamba kauli sahihi kwa dalili ni kuzingatia tafauti za wakati wa kuchomozewa na mwezi, na kwamba hilo linawafikiana na maandiko ya Sharia pamoja na ilmu ya falaki na nyota.

Al Raafi'i kasema katika "*al Falt-hu al 'Aziiz*":

"Ukionekana mwezi katika nchi moja na haukuonekana katika nchi nyengine, itaangaliwa ikiwa nchi mbili hizo zimekaribiana basi hukumu yao ni kama ya nchi moja, na ikiwa moja iko mbali na nyengine basi kuna kauli mbili:"

"(Inayodhihiri mno), nayo ndiyo kauli ya Abu Hanifa -Allah amrehemu-, na ndiyo aliyoichagua Sheikh Abu Haamid, kwamba haiwawajibikii kufunga watu wa nchi nyengine kutokana na yaliyo pokewa kwa Kuraibu kasema, 'Tuliuona mwezi mwandamo huko Sham usiku wa kuamkia

Ijumaa, kisha nikaja Madina, akasema Ibnu Abbaas –Allah awaridhie: Lini mliuona mwezi? Nikasema usiku wa kuamkia Ijumaa. Akasema: Wewe uliuona? Nikasema: Naam, na watu waliuona na wakafunga, na Muawiya kafunga. Akasema: Lakini sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi na kwa hiyo tutaendelea kufunga mpaka tukamilishe idadi au tuuone. Nikasema: Kwani hutosheki na kuona kwa Muawiya? Akasema: Hivi ndivo alivotuamuru Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie'."

"(Kauli ya pili): Inawawajibikia (watu wa nchi nyengine kufunga), nayo ndiyo aliyoichagua Kadhi Abu a'Tayyib na inasimliwa pia kutoka kwa Ahmad; kwasababu ardhi ya dunia imenyooka, na kwa hiyo ukionekana katika nchi mojawapo tutajua kuwa kinachozuia usionekane katika nchi nyengine ni kitu cha ziada siyo kwamba mwezi hauwezi kuonekana."

"Jinsi gani ya kupima umbali baina ya nchi mbili yamezingatiwa katika *'al Kitabu'* masafa ya kupunguza sala kwa safari, na kama hivo imenakiliwa na Imam na Mwenye "*a'Tahdhiib*". Kasema Imam, kama wangalizingatia masafa ambayo inadhihirika ndani yake tafauti katika mandhari za nchi ingalielekea katika maana, lakini huwenda ikawepo tafauti hiyo pamoja na kuwa masafa ya kupunguza sala hayakutimia kwa kuwepo miinuko na mabonde, na huwenda isiwepo tafauti pamoja na kupindukia masafa hayo, hakuna mwenye kusema hivi. Hivo ndivo alivotaja, lakini watu wa Iraqi na a'Saydalaaniy na wengineo wamezingatia alilotamani wakakisia umbali baina ya nchi

mbili kwamba ni kiasi cha kutafautiana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi mfano Iraqi na Hijazi, au Iraqi na Khurasani; na ukaribiano kwamba ni kiasi cha kuto kutafautiana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi mfano Baghdadi na al Kufa, au a'Ray na Qazwini. Na kuna ambao wamezingatia nchi zikiwapo ukanda mmoja na zikiwa ukanda tafauti, na matawi mawili yanapatikana kutokana na jinsi mbili hizo:"

"(Tawi la Kwanza): Kama ameanza kufunga katika nchi moja kisha akasafiri kwenda nchi ya mbali ambako mwezi haukuonekana katika siku yake ya mwanzo; (tukisema) kila nchi ina hukumu yake, je itamlazimu afunge nao (akishatimiza) au afungue, pana rai mbili: Inayodhihiri mno, nayo ndiyo kauli ya al Qaffaal na ndiyo iliyotajwa katika *'al Kitabu'*, kwamba afunge nao kwasababu yeye kwa kuwa amekwenda nchini kwao amechukuwa hukumu yao na amekuwa miongoni mwao, na imepokewa kwamba Ibnu Abbaas –Allah amridhie- 'alimuamuru Kuraibu awafuate watu wa Madina'."

"(Tawi la pili): Kwamba afungue kwasababu yeye ameshika hukumu ya nchi ya mwanzo na kwa hiyo aendelee nayo. Limefananishwa hilo na mwenye kukodishwa mnyama wa kipando; inawajibika alipe ujira kwa pesa za nchi aliyotoka, na katika "*a'Tahdhiib*" kaleta dhana ya kuipa uzito kauli hii. Ama tukizipa nchi zote hukumu moja, itawapasa watu wa nchi aliyokwenda wawafikiane naye ikithibiti kwao hali ya nchi aliyotoka ima kwa kauli yake kutokana na uadilifu wake au kwa njia nyengine na ni juu yao kuilipa siku ya mwanzo. Unaweza kusema kwa kupima na hili kama

angalisafiri kutoka nchi ambako mwezi ulionekana usiku wa kuamkia Ijumaa kwenda nchi ambako mwezi ulionekana usiku wa kuamkia Jumamosi, na mwezi wa Shawwal ukaonekana usiku wa kuamkia Jumamosi basi itawalazimu wale idi pamoja naye hata kama hawakufunga ila siku ishirini na nane na watalipa siku moja. Ama kwa kupima na kauli ya mwanzo hawataangalia kauli yake akisema "niliuona mwezi", hata tukikubali katika kuthibiti mwezi kauli ya muadilifu mmoja."

"Vile vile itakuwa kinyume cha hayo kama angalisafiri kutoka ambako haukuonekana mwezi kwenda ambako ulionekana na wakala idi siku ya ishirini na tisa katika saumu yake. Tukizipa nchi zote hukumu moja au tukisema anapewa hukumu ya nchi aliyokwenda atakula idi pamoja nao na atalipa siku moja; na tusipozipa nchi zote hukumu moja au tukisema anapewa hukumu ya nchi aliyotoka basi haimjuzii kufungua."

"(Tawi la Pili): Kama umeonekana mwezi katika nchi na mtu huyo akaamkia idi hapo kisha meli ikampeleka hadi nchi ya mbali akasudufia watu wa huko wamo katika kufunga, imepokewa kwa Sheikh Abu Haamid kwamba itamlazimu ajizuie kula wakati uliobakia siku hiyo tukisema kwamba kila nchi ina hukumu yake."

"Lakini Imam kaiona kauli hiyo ni mbali na usahihi kwa kuwa hayakuja mapokeo yo yote kuhusiana nayo, kisha kuigawa siku moja ikawajibishwa kujizuilia kula baadhi ya siku hiyo ni mbali na usahihi. Akamfuata katika rai hiyo mwenye *'al Kitabu'* akasema ni baidi kuwajibishwa kujizuia

hadi mwisho wa siku. Lakini Sheikh anaweza kusema kwa nini haifai kuwajibika kujizuia sehemu ya siku? Huoni kuwa mwenye kuamka siku ya thalathini ya Shaaban akiwa hajafunga kisha ukasimama ushahidi juu ya kuonekana kwa mwezi inamwajibikia ajizuie mchana uliobaki?" (mwsh)

Ibnu Aabidiin kasema katika "*Haashiyat raddul mukhtaar*":

"Jua kuwa tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi yenyewe haina mzozo kwa maana ya kwamba inawezekana pakawa baina ya nchi mbili kuna umbali ambao mwezi mwandamo unachomoza usiku kadha katika mojawapo ya nchi mbili hizo pasina nyengine, halikadhalika nyakati za kuchomoza jua zinatafautiana. Kwasababu kuachana mwezi na muale wa jua kunatafautiana kwa mujibu wa tafauti za nchi, hata ikawa jua likipindukia katikati kwenye nchi za mashariki hailazimiki lipindukie katikati wakati huo katika nchi za magharibi. Halikadhalika kuchomoza kwa alfajiri na kuzama kwa jua. Bali kila jua linapotembea daraja moja huwa ni kuchomoza alfajiri kwa watu wa nchi fulani, na kuchomoza jua kwa wengine, na kuzama jua kwa baadhi ya nchi, na nusu ya usiku kwa wengine, kama ilivo katika *'a'Zailai*'."

"Umbali ambao wakati wa kuchomozewa na mwezi unaweza ukatafautiana umekisiwa kuwa ni kuanzia mwendo wa mwezi na zaidi kwa mujibu wa ilivo katika *'al Qahastaniy'* kutoka kwenye *'al Jawaahir'* kwa kuzingatia kisa cha Nabii Sulaiman –amani imshukie-; kwani yeye alikwenda kila asubuhi na jioni kutoka ukanda mmoja hadi ukanda

mwengine wakati mwendo wa baina ya kanda mbili ni mwezi. Na haufichikani udhaifu uliomo katika hoja hiyo."

"Katika *'Sharhu al Minhaaj*' ya a'Ramliy: a'Taaju a'Tabriiziy kazindua kwamba tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi haiwezekani chini ya masafa ya farsakhi ishirini na nne, na hili Baba kalitumia katika fatwa, na inavoelekea masafa hayo yameainishwa kwa uhakika kama alivofutu pia.(mwsh) Basi hilo lihifadhiwe, lakini khilafu imo katika kuzingatia tafauti za wakati wa kuchomozewa na mwezi kwa maana ya kwamba je watu wa kila nchi wanawajibika kuzingatia muandamo wao wala halazimiki mtu kufuata muandamo wa wengine, au haizingatiwi tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi bali inawajibika kufuata waliotangulia kuuona mwezi hata kama umeonekana nchi za mashariki usiku wa kuamkia Ijumaa na nchi za magharibi usiku wa kuamkia Jumamosi watawajibika watu wa nchi za magharibi kufuata walipouona watu wa nchi za mashariki?"

"Kuna waliosema kauli ya kwanza na ndiyo aliyoitegemea a'Zailai na Mwenye *al-Faydh*, nayo ndiyo sahihi kwa madhehebu ya A'Shaafi'i kwasababu kila watu wanaamuriwa kwa mujibu wa hali waliyo nayo kama ilivo katika nyakati za sala. Na kaiunga mkono katika *a'Durar* kwa yale ambayo yametangulia ya kuto kuwajibika isha na witri juu ya mwenye kuukosa wakati wa sala mbili hizo.[1]"(mwsh)

[1] Anaashiria rai ya wale wanao ona kuwa watu wa nchi ziliopo katika ncha ya dunia ya kaskazini au kusini hawa wajibiki kusali isha na witri katika kipindi ambacho jua likizama haupiti ila muda mchache pakawa mapambazuko ya alfajiri

Al Kaasaaniy kasema katika "*Badaai' a'Sanaai'* ":

"Ama yakiwa masafa ni ya mbali baina ya nchi mbili haiwalazimu mojawapo ya nchi hizo hukumu ya nchi ya pili, kwasababu nyakati za kuchomozewa na mwezi za nchi mbali mbali pakiwa baina yake masafa makubwa sana zinatafautiana, na kwa hiyo watu wa kila nchi wanazingatia nyakati za nchi yao za kuchomoza mwezi siyo za nchi nyengine."

Na a'Zaylai' kasema katika *'Tabyiinu al-Haqaaiq*':

"Inavoelekea izingatiwe –yaani tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi- kwasababu watu wa kila nchi wanaamrishwa kwa mujibu wa hali waliyo nayo. Kisha kuachana mwezi na muale wa jua kunatafautiana kwa kutafautiana nchi kama ambavo uingiaji na utokaji wa wakati unatafautiana kwa kutafautiana nchi hizo. Hata jua likipindukia katikati kwenye nchi za mashariki haina maana kuwa wakati huo linapindukia katikati kwenye nchi za magharibi, halikadhalika kuchomoza alfajiri na kuzama jua. Bali kila linapotembea jua daraja moja, basi daraja hiyo ni kuchomoza alfajiri kwa watu wa nchi fulani, na kuchomoza jua kwa wengine, na kuzama jua kwa baadhi ya nchi, na nusu ya usiku kwa wengine."(mwsh)

Na Al-Kamaal bin Al-Humaam kasema katika Sherehe ya 'Fat-hu al-Qadiir' baada ya kuitaja hadithi ya Kuraibu:

"Na hapana shaka kuwa (hadithi) hii ni aula kwasababu ni tamko la wazi kimaana, wakati ile ina

---

yakafuatiwa na jua kuchomoza tena, ambapo wakati wa sala ya isha hukosekana, wakizingatia kuwa watu wa kila nchi wanaamrishwa kwa mujibu wa hali waliyo nayo.

uwezekano wa kuwa maana yake ni kuamrisha watu wa kila penye wakati mmoja wa kuchomozewa na mwezi wafunge kwa uonaji wao wa mwezi".(mwsh)

Na Sheikh Zaadah kasema katika "Majma'u al-Anhur":

"Na (imekuja) kwenye *a'Tabyiin*, inavoelekea izingatiwe kauli hii; kwasababu watu wa kila nchi wanaamrishwa kwa mujibu wa hali waliyo nayo. Kisha mwezi kuachana na muale wa jua kunatafautiana kwa kutafautiana nchi kama ambavo kuingia wakati na kutoka kunatafautiana kwa kutafautiana nchi hizo."(mwsh)

Na kasema katika "*A'Durar*", "Inaungwa mkono na yaliyopita mwanzoni mwa kitabu cha sala ya kwamba sala ya isha na ya witri haiwajibiki kwa yule mwenye kuukosa wakati wa sala mbili hizo.[1]"(mwsh)

Na A'Zubaidiy kasema katika "*It-haafu a'Saadah al-Muttaqiin*":

"Na yawezekana nyakati za kuchomozewa na mwezi zikatafautiana na ikawa kuonekana mwezi katika mojawapo ya nchi mbili kunalazimisha uonekane katika nchi ya pili bila kinyume; na hilo ni kwa kuwa usiku unaingia katika nchi za mashariki kabla kuingia katika nchi za magharibi. Hivo, ikiwa wakati wa kuchomozewa na mwezi ni mmoja (baina ya nchi mbili) inalazimika ukionekana mwezi katika nchi mojawapo uonekane pia katika nchi ya pili. Na ikiwa wakati wa kuchomozewa na mwezi umetafautiana (baina yao) inalazimika ukionekana katika nchi iliyo mashariki

[1] Angalia maelezo ya chini yaliyo tangulia uk 32.

uonekane pia katika nchi iliyo magharibi, wala haiwi kinyume. Basi Sham iko magharibi ya Madina na kwa hiyo hailazimiki ukionekana Sham uonekane Madina; na hivo ndivo inavoonesha hadithi ya Kuraibu..."(mwsh)

Na Sheikh Muhammad Bakhiit Al-Mutii'y –ambaye ni miongoni mwa maulama wakubwa wa madhehebu ya kihanafi wa mwishoni- kasema katika "*Irshaad Ahli al-Milla ilaa Ithbaati al-Ahillah*":

"Nawe ukirejea kwenye hali inayotokea na jambo lenyewe lilivo utakuta kuwa tafauti ya nyakati za kuchomozewa na mwezi na jua (baina ya nchi) ni jambo linalojulikana bila tabu; na kutafautiana nchi katika nyakati kutokana na kutafautiana nyakati zao za kuchomozewa na mwezi na jua ni jambo linaloshuhudiwa na kuonekana. Kwani wakaazi wa nchi ambazo jua linaendelea kudhihiri miezi miwili au mitatu wanalishuhudia hilo, vile vile kila anayekwenda kwenye nchi yao analishuhudia hilo. Kisha imekuwa miongoni mwa yanayojulikana bila tabu kwamba jua linadhihiri miezi sita na linafichikana miezi sita kwa wakaazi wa upande wa pembe ya dunia, je basi inawezekana watu wa Misri wakiuona mwezi wa Ramadhani wakati wa magharibi kwao tuwalazimishe hawa kufunga kwa kuuona watu wa Misri? Aidha, imekuwa ni katika yanayojulikana bila tabu kutafautiana kwa wakati baina yetu na baina ya watu wa Amerika, je inawezekana tuwalazimishe kufunga kwa kuuona mwezi watu wa Misri baada ya magharibi, pamoja na kwamba wakati huu labda kwao utakuwa wakati wa kuchomoza alfajiri au wakati wa kuchomoza jua?"

Kisha kasema:

"Na kwa ujumla kauli ya kuto kuzingatia tafauti za wakati wa kuchomozewa na mwezi na jua inapingana na dalili za kiakili na za kimaandiko. Upingano wake na dalili za kiakili ni kwa yale uliyo yajua ya kupingana kauli hiyo na lile ambalo limethibiti bila shaka la kutafautiana nyakati, na kwamba mchana kwa watu wa nchi fulani huenda ukawa ni usiku kwa wengine. Ama upingano wake na dalili za kimaandiko ni kwa kuwa kauli hiyo inapingana na yaliyotangulia kutoka kwa Kuraibu ..."

KAULI YA IBNU TAIMIA

Ibnu Taimia kasema katika "Fatawa" zake:

"Suala la kuonekana mwezi baadhi ya nchi kuwa sawa na kuonekana kwa nchi zote: lina mgongano; kwani Ibnu Abdil'Barri amenukuu ijmai juu ya kwamba khitilafu imo katika sehemu ambazo inawezekana zikawa na nyakati moja za kuchomozewa na mwezi; ama sehemu zilizo kama al-Andalus na Khurasani (kwa umbali) hakuna khilafu kuwa hakuzingatiwi (kuonekana kwa nchi mojawapo)."

"Nimesema –msemaji ni Ibnu Taimia-: Ahmad ametegemea katika mlango huu hadithi ya bedui aliyeshuhudia kuwa mwezi uliandama usiku uliopita na Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- akawaamuru watu kwa kutegemea muandamo huo pamoja na kwamba ulikuwa si katika mji waliyomo, na haiwezekani ukawa zaidi ya masafa ya safari ya kupunguza sala; wala Mtume hakumtaka bedui huyo atoe maelezo zaidi. Hoja hii haipingani na yale aliyo yataja Ibnu Abdil'Barri; lakini ni

kiasi gani cha masafa kinakubalika kwa hilo? Wale waliosema muandamo huo hauwi kwa nchi zote, kama wengi wa watu wa A'Shaafii'y, baadhi yao wamesema masafa hayo ni masafa ya safari ya kupunguza sala, na baadhi yao wamesema ni kiasi cha masafa ya kukhitalifiana katika wakati wa kuchomozewa na mwezi kama Hijazi na Sham, au Iraqi na Khurasani; na kauli mbili hizo zote ni dhaifu; kwani masafa ya kupunguza sala hayana uhusiano na mwezi. Ama kanda ambazo nchi zimo ndani yake, haikubainishwa ni umbali gani? Kisha kauli mbili hizi ni kosa kwa pande mbili:"

"Upande wa kwanza: Kwamba kuonekana kwa mwezi kunatafautiana kwa kuhitilafiana nchi upande ziliko zikiwa mashariki na nyengine magharibi; kwani mwezi ukionekana nchi za mashariki lazima uonekane pia nchi za magharibi na haiwi kinyume chake; kwasababu wakati wa kuzama jua nchi za magharibi unachelewa mpaka litangulie kuzama nchi za mashariki. Hivyo, ikiwa mwezi umeonekana nchi za mashariki utazidi nuru katika nchi za magharibi na kuwa mbali na jua na mwanga wake wakati linapozama, na kwa hiyo nchi hizi hustahiki zaidi kuuona. Tafauti na hivo ukionekana nchi za magharibi mwanzo, kwasababu inawezekana kuwa sababu ya kuuona ni kuchelewa jua kuzama huko ukazidi mwangaza na kuwa mbali na jua, wakati jua lilipozama nchi za mashariki ulikuwa karibu nalo, kisha ulipoonekana nchi za magharibi ulikuwa umeshazama hauonekani kwa watu wa nchi za mashariki. Hili ni jambo linaloshuhudiwa katika kuzama kwa jua, mwezi na sayari nyenginezo; na kwa hiyo ukiingia wakati wa magharibi

katika nchi za magharibi unakuwa umeshaingia katika nchi za mashariki na haiwi kinyume chake. Vile vile likichomoza jua katika nchi za magharibi linakuwa limeshachomoza katika nchi za mashariki na haiwi kinyume chake; kwani kuchomoza na kuzama kwa nyota na sayari kunatangulia katika nchi za mashariki. Ama mwezi kuchomoza na kuonekana kwake kunatangulia katika nchi za magharibi; kwasababu mwezi unachomoza upande wa magharibi na hakuna mbinguni kinachochomoza upande wa magharibi isipokuwa mwezi; na sababu ya kuonekana ni kuwa mbali na jua, na kwa hiyo kila jua likichelewa kuzama ndiyo mwezi huzidi kuwa mbali nalo."(mwsh)

Kasema aidha:

"Na hoja katika hilo ni kwamba tunajua kwa yakini kuwa mwezi katika zama za Masahaba na Taabiina uliendelea kuonekana katika baadhi ya miji ya Waislamu baada ya kuonekana katika miji yao mingine; hili ni katika mambo ya kawaida ambayo hayabadiliki. Na hapana budi iwafikie habari ndani ya mwezi. Hivyo, ingalikuwa wanawajibikiwa kulipa wangalikuwa wana hima ya kutafuta habari ya kuonekana mwezi katika nchi zote za kiislamu kama walivyokuwa wana hima katika kutafuta habari ya kuonekana mwezi katika nchi yao, na ingalikuwa kulipa ni kwingi katika mingi ya miezi ya Ramadhani. Na jambo kama hili lingalitokea lazima lingalipokewa likasimuliwa; na kwa kuwa halikusimuliwa imeonesha kuwa halina msingi, na hadithi ya Ibnu Abbaas inaonesha hivo."(mwsh)

MAAMUZI YA BARAZA LA FIQHI LA UMOJA WA NCHI ZA KIISLAMU ULIMWENGUNI

Hii ndiyo rai iliyokubaliwa na Baraza la Fiqhi lililo chini ya Umoja wa Nchi za Kiislamu Ulimwenguni, ambalo limetoa maamuzi juu ya hilo kwa makubaliano ya Maulamaa wake wote, ambayo nakunukulia hapa:

"Sifa njema zinamstahikia Allah, na rehma na amani zimshukie yule ambaye hakuna nabii mwengine baada yake."

"Baada ya hayo, Baraza la Fiqhi la Kiislamu limelitafiti suala la tafauti za wakati wa kuchomozewa na mwezi na kutegemeza juu yake uonekanaji wa mwezi, likaona kuwa Uislamu umejengwa juu ya msingi wa kuwa dini ya wepesi na usamehevu, inayokubaliwa na maumbile asilia na akili zilizo sawa kwa kuwa inawafikiana na maslahi ya viumbe. Hivyo, katika suala la miezi miandamo Baraza limechukua rai ya kuithibitisha kwa uonaji wa macho na siyo kwa kutegemea hisabu, kama inavo oneshwa na dalili za kisharia zisizo shaka. Baraza pia limechukua rai ya kuzingatia tafauti za wakati wa kuchomozewa na mwezi (katika kuthibitisha muandamo) kuwa rai hii ina wepesi kwa wakalifiwa pamoja na kuwa ndiyo rai inayo fikiwa na utafiti ulio sahihi. Madai ya wenye kauli inayolazimisha umoja katika siku ya kufunga na ya kufungua yanapingana na yaliyokuja kisharia na kiakili. Ama kisharia, maimamu wa hadithi wametoa hadithi ya Kuraibu: 'Kwamba Ummu al Fadhli bint al Haarith alimtuma kwa Muawiya huko Sham, kasema: nikenda Sham nikamtimizia haja yake, ukaniandamia mwezi niko Sham, nikauona mwezi mwandamo usiku wa kuamkia Ijumaa, kisha nikaja Madina mwisho wa mwezi, akaniuliza Abdalla

bin Abbaas -Allah awaridhie- kisha akautaja mwezi akasema: Lini mliuona mwezi? Nikasema tuliuona usiku wa kuamkia Ijumaa. Akasema: Wewe uliuona? Nikasema: Naam, na watu waliuona na wakafunga, na Muawiya kafunga. Akasema: Lakini sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi na kwa hiyo tutaendelea kufunga mpaka tukamilishe siku thalathini au tuuone. Nikasema: Kwani hutosheki na kuona kwa Muawiya na kufunga kwake? Akasema: La, hivi ndivo alivotuamuru Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie.' (Kaisimulia Muslim katika Sahihi yake)."

"Imam a'Nawawiy katika sherehe yake ya Muslim kaiwekea anuani hadithi hii kwa kusema: (Mlango wa kubainisha kwamba kila nchi wana muandamo wao na kwamba wakiuona mwezi katika nchi mojawapo haithibiti hukumu yake kwa nchi iliyo mbali nao). Na hakuna aliyeacha njia hii miongoni mwa walioitoa hadithi hii kati ya wenye vitabu sita vya hadithi wakiwemo Abu Daud, a'Tirmidhiy na a'Nasaiy katika anuani zao kwa hadithi hii."

"Uislamu umefunganisha hukumu ya kufunga na kufungua na uonaji wa mwezi kwa macho pasina jingine kwa dalili ya yaliyokuja katika hadithi ya Ibnu Umar –Allah awaridhie- kasema: Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- kasema: ((Msifunge mpaka muuone mwezi na msifungue mpaka muuone; mkizingiwa na mawingo msiuone ukadirieni)); kaisimulia al Bukhari na Muslim katika sahihi zao. Hadithi hii imeshurutisha kwa hukumu ya kufunga na kufungua sababu maalumu, nayo ni kuonekana mwezi, ambako huenda kukatokea katika nchi kama Makka

na Madina na kusitokee katika nchi nyengine; kwani unaweza ukawa wakati huo ni mchana kwa wengine vipi wataamrishwa kufunga au kufungua. Ameeleza hayo katika *'Bayaan al adillah fiy ithbaati al ahillah'*. Na maulama kutoka madhehebu zote wameamua kuwa tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi ndiyo inayozingatiwa (katika kuthibitisha mwandamo) kwa wengi, kwani Ibnu Abdil'Barri amesimulia ijmai ya kuto kuzingatia mwezi ulio onekana nchi nyengine kwa nchi zilizotengana sana kwa umbali kama Khurasani kutoka al Andalus, au kila nchi ina hukumu yake peke yake. Na vingi kati ya vitabu vya watu wa madhehebu nne vimejaa maandiko yanayotaja uzingatiaji wa tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi kutokana na dalili zilizosimama katika Sharia juu ya hilo, na vitabu vya fiqhi vitakuonesha yale ambayo yataondoa kiu yako."

"Ama kiakili tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi hakuna ye yote katika maulama mwenye kuipinga kwasababu ni katika mambo yanayoshuhudiwa ambayo akili inayatolea hukumu. Kwa hiyo akili na Sharia vimewafikiana juu ya hilo; kwani vimewafikiana katika kutegemeza nyingi kati ya hukumu juu ya hilo, kati yake ni nyakati za sala. Na tunapoirejea hali halisi inavyokuwa, inatuonesha kuwa tafauti ya wakati wa kuchomozewa na mwezi ni katika mambo yanayotokea kikawaida. Kwa mwangaza huo, Baraza la Fiqhi la Kiislamu limeamua kuwa hakuna haja ya kulingania uunganishwaji wa miezi na Siku ya Idi katika Ulimwengu wa Kiislamu, kwasababu hilo halina dhamana ya umoja wao, kama wanavodhani wengi kati ya wanao lipendekeza, na kwamba suala la kuuthibitisha mwezi

ziachiwe ofisi za fatwa na ukadhi katika nchi za kiislamu, kwasababu kufanya hivo ni aula na inastahiki zaidi kwa maslahi ya umma wa kiislamu; na kwamba linaloleta dhamana ya umoja wa Umma huu na umoja wa neno lake ni kuwafikiana kwao juu ya kukitekeleza Kitabu cha Allah na Sunna ya Mtume Wake –rehma za Allah na amani zimshukie- katika mambo yao yote; na Allah Ndiye Mwenye kuleta mafanikio."

"Na rehma za Allah na amani zimshukie Nabii wetu Muhammad na Aali zake na Sahaba zake."(mwsh)

Maamuzi haya yalipitishwa na maulama waliohudhuria katika kikao cha Baraza hilo, sawa wakiwa Wasaudia kama Sheikh al Harakan, ambaye alikuwa katibu mkuu wa Baraza hilo, na Masheikh wawili Ibnu Humaid na Ibnu Baz, au waliokuja kutoka nje ya nchi ya Saudi Arabia kama Sheikh Abu al Hasan a'Nadawiy.

IDI YA AL-ADH-HA (YA AL-HAJJ) NI SAWA NA IDI YA AL-FITRI KATIKA HUKUMU YA KUTHIBITI KWA MUANDAMO WA NCHI INAYOZINGATIWA

Nawe unaona kuwa wao wamezitaja idi kwa ujumla na hawaku tafautisha baina ya idi al fitri na idi al adh-ha, kwani kila moja kati ya idi mbili hizo unahisabiwa wakati wake kwa kuuona mwezi katika nchi yenyewe waliomo watu au katika nchi inayowafikiana nayo katika wakati wa kuchomoewa na mwezi, au kwa kukamilisha idadi ya siku thalathini. Idul-fitri inathibiti hukumu yake kwa kuuona mwezi muandamo wa Shawwal au kumalizika idadi ya siku

thalathini za Ramadhan, na Idul-adh-ha inathibiti hukumu yake baada ya kupita siku tisa tangu kuonekana mwezi wa Dhul-hijjah au tangu kumalizika idadi ya siku thalathini za mwezi wa Dhul-Qa'dah. Haya ndiyo yanayo kubaliana na dalili za kiakili na za kimaandiko kama itakavokuja insha Allah.

Kisha Mwanachuoni Mkubwa Sheikh Abdallah bin Humaid ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Mambo ya Misikiti Miwili Mitukufu (wa Makka na wa Madina) ametunga makala maalumu aliyo yaita "*Tibyaanu al Adillah fiy Ithbaati al Ahillah*" (Ubainisho wa Dalili katika Kuthibitisha Miezi miandamo), ambamo anawapinga wale wanaonadia uunganishwaji wa miezi miandamo iwe sawa katika Ulimwengu wa Kiislamu, akabainisha katika makala hayo kosa la kulingania jambo hilo kwa kuwa linapingana na dalili za kiakili na za kimaandiko, na miongoni mwa yale aliyosema kwenye makala yake hayo:

"Nikatoa upinzani wa kuwa hili haliwafikiani na hadithi sahihi kutoka kwa Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie, wala haliwafikiani na rai ya wengi kati ya maulama wahakiki wa Kihanafi, Kimaaliki, Kishaafi'i na Kihanbali, wala halikubaliani na yanayo wafikiana na ilmu ya nyota na Jografia ya kisasa, hata kama rai waliyochukua baadhi ya wajumbe wa Baraza, ya kulazimika watu wote duniani kufunga na kufungua kwa kuonekana mwezi katika nchi mojawapo, ni rai ya baadhi ya maulama, lakini haikutegemea dalili inayoiunga mkono si kiakili wala kimaandiko; bali ni katika yanayojulikana bila tabu kuto kusihi kwa kauli hii – kama utakavoona."

"Kwa ajili hiyo, nimeona niandike kuhusiana na maudhui hii makala yenye kuibainisha haki na kuliweka wazi kusudio, na kwamba nyakati za kuchomozewa na mwezi zinatafautiana (baina ya nchi) kwa maafikiano ya wenye ilmu, na kwa hiyo kila watu wa nchi wana uonaji wao wa mwezi kwa namna itakavo fafanuliwa ..."

Na baada ya kuitaja hadithi ya Kuraibu kasema:

"Na hii inataja wazi kwamba kila nchi ina uonaji wake wa mwezi, na kauli ya Ibnu Abbaas, 'Hivi ndivo alivotuamuru Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie' inaonesha kuwa ni amri iliyothibiti kutoka kwa Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- kuhusiana na hilo. Wala hakuikataa Ibnu Abbas habari ya Kuraibu kwa kuwa ni habari ya mtu mmoja; kwani kama ingalikuwa ni hivo angalimwandikia Muawiya akamuuliza kuhusu kuonekana mwezi kwake, au Muawiya angaliwaandikia watu wa Madina kuwapa habari ya kuthibiti kuonekana mwezi kwao usiku wa kuamkia Ijumaa kwa ajili ya kuilipa ile siku ambayo hawakuifunga. Na kwa kuwa hakuna lilokuwa kati ya hayo, imeonesha kuwa kila nchi ina uonaji wake wa mwezi kama ilivokuwa ikijulikana wakati wa Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- na wakati wa makhalifa wake; kwani wao hawakuwa waki iandikia miji wala watu wa miji hawakuwa wakiwaandikia kuhusu uonekanaji wa mwezi kwao, juu ya hima yao kubwa katika dini na pupa lao juu ya mambo ya kheri."(mwsh)

Kisha akaingia katika kunukuu maneno ya maulama wahakiki wa Madhehebu Nne yanayo onesha kuwa hii ndiyo

haki, akataja pia waliyosema maulama kuhusiana na tafauti ya nyakati za kuchomozewa na mwezi na jua (baina ya nchi) na athari yake juu ya tafauti ya mianzo na miisho ya miezi.

FATWA ZA MAULAMA WA SAUDI ARABIA KUHUSU TAFAUTI YA MUANDAMO

Wengi kati ya maulama wa Saudi Arabia wametaja wazi katika fatwa na vitabu vyao kuwa kauli yao ni hii.

FATWA YA SHEIKH IBNU UTHAIMIN

Sheikh Ibnu Uthaimin ana fatwa nyingi katika maudhui hii, yamekuja katika baadhi ya fatwa hizo yafuatayo:

"Maulama -Allah awarehemu- wamekhitalifiana kuhusu iwapo mwezi umeonekana pahala pamojawapo katika nchi za waislamu pasina kwengineko, je inawalazimu waislamu wote kufuata mwandamo huo, ama hauwalazimu isipokuwa waliouona na wanaowafikiana nao katika wakati wa kuchomozewa na mwezi, au waliouona na walio pamoja na wao chini ya utawala mmoja; kuna kauli kadha katika hilo; pia kuna khilafu ya namna nyengine."

"Na kauli yenye nguvu ni kwamba panarejewa watu wa maarifa, ikiwa nyakati za kuchomozewa na mwezi katika nchi mbili zinawafikiana, zitakuwa kama nchi moja: ukionekana mwezi katika mojawapo ya nchi mbili hizo, itathibiti hukumu yake katika nchi ya pili. Ama ikiwa nyakati za kuchomozewa na mwezi zinatafautiana, kila nchi itakuwa na hukumu yake yenyewe, na hii ndiyo kauli aliyochagua Sheikh al Islam Ibnu Taimia –Allah amrehemu- nayo ndiyo dhahiri ya Kitabu cha Allah na Sunna na inavooneshwa na Qiyasi."

"Ama Kitabu cha Allah, kasema Allah Taala:

((...فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ وَمَنْ كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَى مَا هَدَاكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ))

[...Basi atayeushuhudia (atayeuhudhuria nchini kwake) mwezi huu na aufunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu katika siku nyengine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hisabu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongoeni na ili mpate kushukuru] (Albaqara: 185). Yanayofahamika kutokana na aya hii ni kwamba asiyeushuhudia nchini kwake haitamlazimu kufunga."

"Ama Sunna, kasema Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie, 'Mkiuona fungeni, na mkiuona fungueni.' Yanayofahamika kutokana na hadithi hii: iwapo hamkuuona haitalazimu kufunga wala kufungua."

"Na qiyasi ni kwasababu wakati wa kujizuilia kula na wa kufutari unazingatiwa katika kila nchi peke yake pamoja na nchi itakayowafikiana nayo katika machweo na mawio, na hili ni jambo lilokubaliwa na wote. Utaona watu wa mashariki ya Asia wanajizuilia kula kabla watu wa magharibi yake na wanafutari kabla yao, kwasababu alfajiri inachomoza kwa wale kabla hawa; vilevile jua linazama kwa wale kabla hawa. Na ikiwa limethibiti hili katika kujizuilia kula na kufutari kwa kila siku basi na iwe kama hivo katika kufunga na kufungua kwa mwezi mzima wala hapana tafauti."

"Lakini nchi zikiwa chini ya utawala mmoja, na mtawala wa nchi hizo akaamuru watu wafunge au wafungue

italazimu kufuata amri yake; kwasababu suala ni la khilafu, na hukumu ya mtawala inaondoa mzozo."

"Kwa msingi huo, fungeni na fungueni kama wanavofunga na kufungua watu wa nchi mliyomo nyinyi, sawa ikiwa imewafikiana na nchi yenu ya asli au haikuwafikiana. Vilevile siku ya Arafa fuateni nchi mliyomo nyinyi."

Na aliulizwa kuhusu wanaonadia uunganishwaji wa Umma (wa kiislamu) katika saumu na ufunganishwaji wa nyakati za nchi zote za kuchomozewa na mwezi kwa nyakati za Makka akasema:

"Hili kwa upande wa kifalaki ni muhali, haliyumkiniki; kwasababu nyakati za kuchomozewa na mwezi - kama alivosema Sheikh al Islam Ibnu Taimia Allah amrehemu- zinatafautiana (baina ya nchi) kwa mawafikiano ya wenye maarifa ya ilmu hii; na zikiwa zinatafautiana basi zinavo onesha dalili za kimapokeo na za kitaalamu ni kwamba kila nchi ipewe hukumu yake peke yake."

FATWA YA SHEIKH IBNU BAZ

Imekuja katika fatwa ya Sheikh Ibnu Baz yafuatayo:

"Na kundi katika wenye ilmu wanaona kuwa kila nchi ina uonaji wake wa mwezi zikitafautiana katika nyakati za kuchomozewa na mwezi. Na wametoa hoja kwa yaliyothibiti kutoka kwa Ibnu Abbaas -Allah awaridhie- kuwa yeye hakufuata uonaji wa watu wa Sham, na alikuwa Madina - Allah amridhie, na watu wa Sham walikuwa wameuona mwezi usiku wa kuamkia Ijumaa na wakafunga kwa hilo

katika zama za Muawia –Allah amridhie; ama watu wa Madina hawakuuona ila usiku wa kuamkia Jumamosi; akasema Ibnu Abbaas –Allah awaridhie- wakati Kuraibu alipompa habari ya kuuona mwezi watu wa Sham na kufunga kwao, "Sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi na kwa hiyo tutaendelea kufunga mpaka tuuone au tukamilishe idadi".

"Ametoa hoja kwa kauli ya Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie, 'Fungeni kwa kuuona na fungueni kwa kuuona' - hadithi. Hii ni kauli yenye kiasi chake cha nguvu, na wameichagua wajumbe wa Baraza la Umoja wa Maulama Wakubwa katika Saudi Arabia ili kuoanisha baina ya dalili mbali mbali, na Allah Ndiye Mwenye kuleta mafanikio".(mwsh)

Kasema pia:

"Wamesema kundi katika maulama: hukumu ya kuonekana kwa mwezi inajumuisha nchi nyengine ikiwa nyakati zao za kuchomozewa na mwezi ni moja, ama zikitafautiana basi kila watu wenye wakati mmoja wa kuchomozewa na mwezi wana uonaji wao wa mwezi. Imam a'Tirmidhi –Allah amrehemu- kaisimulia kauli hii kutoka kwa wenye ilmu, na wameitolea hoja kwa yale aliyoyatoa Muslim katika sahihi yake, 'Imepokewa kwa Ibnu Abbaas –Allah awaridhie- kuwa Kuraibu alimjia Madina kutoka Sham katika mwisho wa Ramadhani, akampa habari kwamba mwezi ulionekana huko Sham usiku wa kuamkia Ijumaa, na kwamba Muawiya na watu wamefunga kwa mwezi huo. Ibnu Abbaas akasema: Lakini sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi, na kwa hiyo tutaendelea kufunga

mpaka tuuone au tukamilishe idadi. Kuraibu akamwambia: Kwani hutosheki na kuuona kwa Muawiya na kufunga kwake? Akasema: La, hivi ndivo alivotuamuru Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie'. Wamesema hii inaonesha kuwa Ibnu Abbaas anaona kuwa kuonekana kwa mwezi hakujumuishi nchi zote, na kwamba kila watu wa nchi wana uonaji wao zinapotafautiana nyakati za kuchomozewa na mwezi, na wakasema nyakati za kuchomoza mwezi katika eneo la Madina hazikuungana na nyakati za kuchomoza mwezi za Sham".

Kasema pia:

"Zaidi ya hayo, inapasa kutanabahi kuwa uzingatiaji wa tafauti za wakati wa kuchomozewa na mwezi ni katika masuala ambayo imetokea ndani yake khilafu baina ya wenye ilmu, na Umoja wa Maulama Wakubwa umelitafiti suala hili katika mmoja wa mikutano yake ya kawaida iliyopita na ukachukua azimio kwa wingi wa wenye kuunga mkono, linalomaanisha: kuwa yenye nguvu zaidi ni kauli ya wenye kusema kwamba kila nchi ina uonaji wake wa mwezi na ni juu yao warejee kwa maulama wao katika hilo, ili kufuata yaliyopokewa na Muslim katika sahihi yake ambayo ni hadithi ya Kuraibu kutoka kwa Ibnu Abbaas".(mwsh)

KAULI ZA MASHEIKH WENGINEO WA SAUDI ARABIA

Sheikh Saleh Alfawzan kasema, "Na hilo linatafautiana kwa tafauti za nyakati za kuchomozewa na mwezi kwa iliyo sahihi katika kauli mbili za maulama".

Na Sheikh Yusuf bin Ahmed Alqaasim, mjumbe wa Umoja wa Walimu katika Chuo cha Elimu ya Juu cha Ukadhi huko Saudi Arabia kasema, "Na yenye nguvu zaidi katika kauli zilizosemwa: kwamba kila nchi ina uonaji wake wa mwezi, hususan pakiwa na tafauti ya nyakati za kuchomozewa na mwezi".

Na Sheikh Alhaaj Muhammad bin Abdil-Wahhaab bin Abdi'Razzaaq –akiwajibu wanao ona kuwa kuto kuungana waislamu kwa idi na minasaba mengineyo kuna mfarakano katika Dini – kasema yafuatayo:

"Ni wazi kwamba lugha ya muandishi huyu inamaanisha kwamba kuungana kwa idi na minasaba mengineyo daima ni jambo linalo amrishwa kisharia na kiakili, na kwamba kutafautiana katika hayo kunapingana na umoja unaotakiwa na kunapingana na Sharia pamoja na akili. Na hili si sahihi, kutokana na uliyo yajua kwamba kuungana katika hayo daima katika nchi zote hakuwezekani kisharia wala kiakili, na kwamba kutafautiana katika hayo hakuhesabiki kuwa kunapinga umoja unaotakiwa, na zimetangulia miongoni mwa dalili juu ya hayo zile ambazo zinatosha. Hata hivo, yote aliyo yataja muandishi huyu hapa hayakubaliki, bali ni yenye kupingana na dalili za kiakili na za kimaandiko, nami nakubainishia hayo kwa kusema:"

"Kauli yake: 'Itaingiaje akilini kuwa mataifa ambayo yanajumuishwa na uhusiano wa Uislamu na umoja wa dini yawe yanatafautiana katika kielelezo cha uhusiano huu na anuani ya umoja huo?'."

"Ni wazi kuwa haya ni maneno ambayo yamekuja si pahala pake; kwasababu suala hili si katika masuala ambayo Mweka Sharia katulazimisha tuyafanye wakati mmoja nchi zote hata isemwe itaingiaje akilini...; bali tulicho lazimishwa ni kufunga na kufungua – kwa mfano - baada ya kuuona mwezi kutokana na kauli yake –rehma za Allah na amani zimshukie: 'Msifunge mpaka muuone mwezi...', na kauli yake: 'Watu wa kila nchi wana uonaji wao wa mwezi'. Na umeshajua kutokana na maneno ya Al Qarraafi na wengine kuwa uonaji wa mwezi unaweza ukatafautiana kwa siku moja kwasababu ya nchi kuwa mbali na nyengine. Vile vile muungano wa idi na mengineyo katika nchi zote, hali ya kifalaki ilivo haisaidii kuuleta; kwasababu tukichukulia kuwa mwanzo wa idi – kwa mfano – tokea kuzama kwa jua katika upeo wa Moroko, basi wakati huo kwa wengine yawezekana ukawa nusu ya usiku, au wakati wa alfajiri, au wa kuchomoza jua, au wa kupindukia jua. Ikichukuliwa kwamba jua wakati huo lilikuwa mwanzoni mwa burju ya Hamal au Mizani, basi kuzama kwa jua katika nchi zote wakati huo kunakuwa saa kumi na mbili jioni na hapana tatizo. Ukifika wakati wa kuzama jua katika nchi ya Moroko, ambao ni saa kumi na mbili jioni, wakati huo katika nchi ya Tunisia itakuwa ni saa 1 na dakika 12 usiku, na Bombai India ni saa 5 na dakika 23 usiku, na Tokyo Japan ni saa 9

na dakika 51 baada ya nusu ya usiku, na Hawai ni saa 2 na dakika 12 asubuhi, na New York ni saa 7 na dakika 35 baada ya adhuhuri. Utawezekanaje muungano pamoja na tafauti hii, kwani neno muungano linamaanisha kuwafikiana katika kuanza na kumaliza. Juu ya hivyo, tukiuhisabu muungano katika suala hili kuwa ni jambo la lazima, ni nchi gani ambayo inapasa uzingatiwe uonaji wake wa mwezi na uzamaji wake wa jua? Na tukijaalia kuwa ni nchi fulani je nini ambacho kimeifanya itangulizwe kuliko nchi nyenginezo?"

"Vile vile kwa nini tusiseme hilo kuhusu nyakati za sala pamoja na kuwa sala ni kielelezo cha mshikamano wa kiislamu na ni anuani ya umoja iliyo wazi kuliko vyenginevo vyote, kwani sala ni nguzo kuu ya Uislamu baada ya tamko la shahada. Aidha, ikiwa miezi na siku zisizo za kiarabu zinatafautiana kwa sehemu ya siku kwa vile mwanzo wa siku ni kuanzia nusu ya usiku wa nchi, itakuwaje kwa miezi na siku za kiarabu zinazotegemea kuzama kwa jua na kuonekana kwa mwezi muandamo jioni?..."(mwsh).

WINGI WA MAANDIKO YA MAULAMA KATIKA RAI HII

Kwa ujumla, maandiko ya maulama katika rai hii ni mengi kiasi ambacho siwezi kuyataja yote, na kama ningeyafuata nikaku kusanyia yote yangalifanya kitabu kikubwa sana, na yote yanaonesha kuwa kauli iliyothibiti kwa dalili ni kwamba tafauti za nyakati za kuchomozewa na mwezi zinaathiri hukumu za miezi muandamo na hukumu za kisharia zinazo fungamanishwa na miezi hiyo.

Inanitosha kuashiria maandiko yaliyo mbele yangu hivi sasa. Kati yake ni maandiko ya Sheikh Saleh bin Ibrahim Al Bulaihiy katika kitabu chake "*a'Salsabiil fiy Ma'rifat a'Daliil*", na Sheikh Abdu'Rahman bin Qasim Al 'Asimiy katika "*Haashiyat a'Raudh al Murbi' 'ala Zaadi al Mustaqni'*", na Sheikh Abdu'Razzaaq 'Afiifiy katika "*Fatawa*" zake, na Sheikh Abdallah bin Abdulaziz bin 'Aqiil katika "*Fatawa*" zake, na Sheikh Abdallah bin Abdu'Rahman Aljabrin katika "*Fatawa a'Siyam*", na Sheikh Ahmad bin Yahya A'Najmiy katika "*Ta'sis al Ahkam fiima sahha 'an Khairi al Anaam*", na Sheikh Abdallah Sulaiman bin Manii'u katika "*Majmu'u Fatawa*" zake, Sheikh Saleh bin Fauzan katika "*Tas-hil al Ilmam bifiqhi al Ahaadithi min Buluughi al Maraam*", na Sheikh Abdallah bin Saleh Al Fauzan katika "*Fiqhu a'Daliil*", na Sheikh Abdallah bin Abdallah Aljabrin katika "*Sharhu 'Umdat al Fiqhi*", na Masheikhe: Abdallah bin Muhammad bin Ahmad A'Tayyar, na Ibrahim bin Abdulaziz Alghusn, na Khalid bin Muhammad bin Ali Al Mushaiqih katika maelezo yao ya "*A'Raudh al Murbi*' ", na Sheih Abdulkarim A'Namla katika "*Taysir Masaail alfiqhi Sharh a'Raudh al Murbi*'", na Sheikh Zaid bin Muhammad bin Haadi Al Madkhaliy katika "*al Afnaan a'Nadiyya Sharhu Mandhuumat a'Subul a'Sawiyya lifiqhi a'Sunan al Marwiyya*", na Sheikh Muflih bin Ali Al Shamriy katika "*al Badru a'Tamaam*", na Sheikh Khalid bin Ali Al Mardhiy Al Ghaamidiy katika kitabu "*a'Siyaam Masaail wa Ahkaam*", na Sheikh Muhammad Al Mukhtaar bin Muhammad Al Amin

a'Shanqiitiy katika "*Sharhu Zaadi al Mustaqni*'", na Sheikh Muhammad bin Ali bin Adam bin Musa al Aytuubiy katika "*Dhakhiirat al 'Uqba fiy Sharhi al Mujtaba*", na fatwa nyingi za Tume ya Kudumu ya Tafiti za Kitaalamu na Utoaji Fatwa ya Saudi Arabia.

KAULI YA IBNU ABBAAS KATIKA KADHIYA HII SI IJTIHADI KUTOKA KWAKE

Ama uliyoashiria katika barua yako ya kwamba hadithi ya Kuraibu haizidi kuliko kuwa ni ijtihadi ya Ibnu Abbaas –Allah awaridhie-, na kwamba ijtihadi hiyo kamwe si hoja kwasababu yeye ametegemea hadithi isemayo "Msifunge mpaka muuone mwezi ...", hayo ni maneno ya ajabu; kwani ni katika yanayojulikana kuwa kauli ya sahaba, "Tulikuwa tunaamrishwa kadha" au "Tulikuwa tunakatazwa kadha" huwa ina hukumu ya (marfu'u) kuwa imetokana na Mtume, halikadhalika kauli ya sahaba, "Tumeamrishwa" au "Tumekatazwa". Bali imesemwa kuwa Taabii (aliyefuatia masahaba) anaposema hivo inaonesha kuwa hicho ni kitu alichokisikia kwa masahaba na kwa hiyo hupewa hukumu ya hadithi mauqufu (iliyomalizikia kwa sahaba). Na ikiwa hayo ni pamoja na sahaba huyo kuto kutaja kwa uwazi kuwa muamrishaji au mkatazaji ni Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie-, itukuaje kwa yale ambayo ametaja kwa uwazi ndani yake hilo?! Je unadhani kutaja kwa uwazi kuwa muamrishaji ni Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- kunadhoofisha hoja ya kauli hiyo hata iwe yale ambayo hakutaja kwa uwazi hilo ndiyo yana nguvu zaidi kihoja kuliko yaliyotajwa kwa uwazi?!

Chukulia kuwa mambo ni kama ulivosema, lakini Ibnu Abbas hakusema maneno haya pasipokuwapo wale ambao wakisongamana naye miongoni mwa wenye ilmu, bali kayasema katika mji wa Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- kunako songomana nyayo za masahaba –Allah awaridhie- na hakuna yeyote aliyemkana. Kama angalimkana yeyote kungalikuwa kuna sababu za kutosha kusimulia ukanaji wake, lakini hakuna shaka kuwa kunyamazia kwao yale aliyoyasema kunahisabika kuwa ni maafikiano (ijmai) ya kimya, nayo ni hoja inayotegemewa katika masuala ya kiijtihadi.

Zaidi hayo, Ibnu Abbas –Allah awaridhie- alikuwa miongoni mwa masahaba wapana mno kwa ilmu, wakali mno kwa fahamu na waliotopea mno kwa maarifa. Yakutosha kuwa Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- alimuombea Mwenyezi Mungu ampe fahamu ya dini na amuelimishe taawili, na akawa mfasiri wa Qur'ani na bahari ya ilmu isiyofikiwa kina. Nani kwa hiyo anayeweza kumfikia daraja yake hata ampinge kwa pingamizi kama hii?! Je unadhani yeye alikuwa juha hafahamu maana ya yale aliyoyapokea kwa Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- hata aseme anayo yasema bila kujua wala kuhakikisha?!

Nawe umeona waliyo yabainisha maulama ya kwamba maneno yake hayo ni ushahidi ulio wazi katika suala hili, na hilo linatosha kwa hoja. Wala hapana shaka kwamba kauli ya sahaba ikiwa haikupingwa na kauli ya sahaba mwengine haipasi ipingwe kutokana na cheo walicho nacho masahaba;

kwa vile wao waliishi pamoja na Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- wakapata katika utukufu wa usuhuba wake wasicho pata wengineo, na wakachota katika bahari ya ilmu yake wasicho chota wengineo. Umma wote unawategemea wao, na wao wanastahiki mno kufuatwa na wote wale waliokuja baada yao. Inapowafalia watu wa ijtihadi kufanya ijtihadi ni katika yale yaliyopokewa kutoka kwa masahaba iwapo wamekhitalifiana baina yao.

Wala hakuna tatizo katika kuto kuainisha kwake masafa yanayo tenganisha baina ya nchi tafauti katika kupelekea baadhi yake zisifuate uonaji mwezi wa baadhi nyengine, kwasababu kauli yake hiyo ilikuwa katika masafa yanayo tenganisha Sham na Madina; na imejulikana kwa dalili za maandiko zisizo shaka kwamba kupaswa kufunga au kufungua kisharia kunategemea kuthibiti kwa uonekano wa mwezi; na imejulikana kwa ilmu ya yakini kuwa kutafautiana nchi katika nyakati za kuchomoza mwezi kunaathiri katika uwezekano wa kuuona, ikawa unaonekana pahala fulani wakati haiwezekani kuonekana pahala pengine. Hilo ni katika yanayo fasiri kauli yake na kwa hiyo haishurutishwi aainishe masafa yanayo wajibisha kuwe na tafauti ya hukumu katika suala hili. Maulama wa falaki wanaona kuwa mtengano baina ya nchi mbili wa masafa ya maili mia tano unaathiri katika uwezekano wa kuuona mwezi na kuto kuwezekana. Na kwa hili inaondoka pingimizi juu yetu ya kwamba Omani ni nchi kubwa sana, na kwa sababu hiyo inatafautiana pia katika nyakati za sala; kwasababu kutafautiana huku hakupelekei kikawaida kutafautiana katika uwezekano wa kuuona mwezi. Kisha maulama

wamesema kwamba kutafautiana nyakati za kuchomoza mwezi kukiwa kudogo baina ya nchi kiasi cha kwamba haifikiriwi kuwa mwezi utafichikana katika nchi hizo wakati unaonekana katika baadhi yake ila kwa jambo lisilo la msingi hakuzingatiwi. Na baadhi ya haya yamekwisha tangulia katika niliyo nukuu. Hata hivo kutoa hoja kwa kuto kuungana nyakati za sala sikukufanya mimi peke yangu; wangapi wametoa hoja kwa hilo miongoni mwa waliotangulia na wanaoishi zama zetu.

HADITHI YA "HIJJA NI ARAFA" SI DALILI YA KUWA MWEZI WA DHUL-HIJJA UNA HUKUMU PEKEE

Ama kuitolea dalili rai yako - ya kwamba mwezi wa Dhulhijja una hali makhsusi ambapo inawajibika kutegemewe kuthibiti kwa uonekano wa mwezi katika Ummul-Qura – kwa "kuwa hijja ni Arafa, na Arafa ipo Ummul-Qura", hiyo ni hoja ya ajabu, kwasababu linalo julikana kwa watu wa mantiki ni kwamba umaanishaji wa tamko kwa maana fulani ama utakuwa ni umaanishaji kamili au wa kugusia au wa kulazimika, na hivo ndivo walivofuata wengi wa watu wa usuli. Mahanafi kati yao wamezigawa dalili mafungu manne: inayomaanisha kwa tamko lake, inayomaanisha kwa kuashiria, inayomaanisha kwa kubidi na inayomaanisha kwa kuonyesha. Nami siioni hoja hiyo kuwafikiana na lo lote kati ya hayo. Kwani hijja kuwa ni Arafa haina maana kwamba watu wa mbali wanalazimika wategemee uonekanaji wa mwezi wa Dhulhijja

katika Nchi Tukufu ya Makka. Na Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- ameifasiri kwa yale ambayo yanamaanisha kwamba linalo kusudiwa ni kwamba mwenye kuwahi kusimama Arafa japo muda mchache sawa ikiwa kabla ya jua kuzama siku ya Arafa au baada ya jua kuzama usiku wa kulala Muzdalafa, hijja haikumfutu; tafauti na kama angalikuja Arafati baada ya alfajiri ya siku ya kuchinja. Imepokewa kwa Abdur-Rahman bin Ya'mar a'Diiliy kasema: Nimemsikia Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- anasema: "Hija ni Arafa, mwenye kudiriki kufika Arafa usiku wa kulala Muzdalafa kabla ya kuchomoza alfajiri amewahi hija ..." Kaipokea a'Tirmidhi, Abu Daud, a'Nasai, Ibnu Majah, a'Daarami, Ibnu Khuzaima, Al-Baihaqi, Al-Haakim na a'Tabarani, na kasema a'Tirmidhi: Hii ni hadithi hasan, sahih.

Je unaona katika haya yanayo onesha kuwa watu wanalazimika wachukue wakati wa kuingia kwa mwezi wa Dhulhijja kwao kwa mujibu wa watakavo uona mwezi watu wa Makka? Unadhaniaje iwapo mwezi umeonekana nchi za mbali kabla ya kuuona watu wa Makka, je watawajibika wapuuze uonaji huo na wategemee uonaji utakaothibiti kwa watu wa Makka ili tarehe ya Dhulhijja kwao iwe sawa na ya Makka?!!

Pamoja na ubainisho huu wa Mtume wa maana ya "Hija ni Arafa", sioni haja ya kujaza kurasa kwa kauli za washereheshi wa Sunna kuhusiana na maana ya ibara hiyo katika hadithi, na kubainisha kwamba haimaanishi kwa hali yo yote rai uliyoitolea hoja kwa ibara hiyo; kwani hakuna

baada ya ubainisho wa Mtume ubainisho mwengine, na "Ukija mto wa Allah hubatilika mto wa Ma'qil".

Mangapi katika yanayopaswa kuepukwa kisharia hutokea ikiwa mwanzo wa mwezi wa Dhulhijja utafanywa kwa mujibu wa uonekanaji wa mwezi huko Makka Tukufu; kati ya hayo ni:

- Kama umetangulia kuonekana katika nchi fulani, ukachelewa kuonekana huko Makka, na wakafunga siku ya kusimama mahujaji huko Arafa itabidi funga yao iwe tarehe kumi kwa mujibu wa mpangilio wao wa siku wa kawaida, nayo ni siku ya idi iliyoharamishwa kufungwa kwa makubaliano ya wote. Je unadhani vipi itakubalika wafunge tarehe kumi kwa ajili ya kuwafikiana funga yao na kusimama mahujaji Arafa?! Na kama wamechelewa kuuona mwezi kuliko watu wa Makka wakawafuata watu wa Makka katika wakati wao, itabidi wasali idi tarehe tisa kwao na kwa hiyo iwe ni haramu kwao kuifunga siku hiyo, igeuke badala ya kuwa kuifunga ni ibada na kujikurubisha kwa Allah iwe ni haramu. Nawe unajua kuwa hukumu hizi zote zimefungamanishwa na miezi miandamo kwa kuthibiti kuonekana au kutokuthibiti, kama inavo onesha hivo kauli ya Allah Taala:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ))

[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija] (Albaqara: 189), pamoja na yaliyotangulia kubainishwa ya kwamba tafauti za nyakati za kuchomoza mwezi husababisha tafauti ya kuonekana kwa mwezi muandamo, jambo ambalo linategemewa na hukumu za kisharia katika mwezi.

- Vile vile unaweza kuwa mwezi wa Dhulqa'da umechelewa kwao kuliko kwa watu wa Makka, na kwa hiyo wakiuona mwezi kwao watu wa Makka siku ya ishirini na tisa na wao wakawafuata kwa uonaji wao, utakuwa mwezi wao wa Dhulqa'da siku ishirini na nane. Wasipouona siku ya ishirini na tisa kwa mujibu wa tarehe yao ya kawaida waliyo iacha kuwafuata watu wa Makka itapelekea uwe mwezi wa Dhulhijja kwao siku thalathini na moja. Mwezi muandamo utakuwaje chini ya siku ishirini na tisa au zaidi ya siku thalathini?! Tatizo hili limetokea kwetu Oman kwasababu ya ufuataji huu, na hili ni katika yanayo sababisha ubabaifu katika nyingi za ibada za kisharia, kama eda za wake na muda wa kiapo cha kumgomea mke na mengineyo.

Kwa ujumla, kuupa mwezi wa Dhulhijja hukumu ya peke yake ya kwamba uwe kwa mujibu wa uonaji mwezi wa watu wa Makka kunatatiza mno kuliko kusema miezi yote iwe sawa sehemu zote duniani. Kwani kauli hii ingawa haina nguvu, na dalili za kisharia, kimaumbile na kiakili zinaonesha kinyume chake, lakini haipelekei kwenye matatizo ya kidini kama kauli ya kuupa mwezi wa Dhulhujja pekee hukumu hii pasina miezi mengineyo.

Kwa haya inabainika kuwa hoja yako ya kwamba "Hija ni Arafa" na Arafa ipo katika vitongoji vya Makka, ni hoja yenye nguvu mno katika kuyavunja haya unayo yaashiria na kuyataka - ya kuwaunganisha watu wa nchi za mbali na watu wa Makka katika mwezi wao; kwani hakuna hijja kwenye hizo nchi za mbali, na watu huko hawatakiwi waabudu kwa lolote kati ya ibada za hijja katika miezi ya hijja, bali haiwafalii kufanya hivo; haiwapasi waliobaki nchini kwao huko na hawakuwa miongoni mwa mahujaji kuvaa ihramu wala kutufu wala kusai wala kutupa vijiwe, kwasababu ibada hizi zote hazifanywi isipokuwa kwenye yale maeneo matukufu ya Makka pasina nchi nyengine za mbali. Watu wa Makka wenyewe hawatakiwi kufanya cho chote kati ya hayo isipokuwa waliohirimia hijja. Lakini sababu ya kuwa hukumu yao katika mwezi ni kama hukumu ya mahujaji ni kwa kuwa muandamo wa mwezi ni jambo la kimaumbile linalo ambatana na hukumu za kisharia. Kuwepo kwao pamoja na mahujaji kwenye nchi moja kumekuwa sababu ya kuungana nao hata kama hawakutoka pamoja nao kwenda kwenye sehemu za ibada za hija, kwasababu mwezi wao

kimaumbile na kisharia ni mwezi mmoja, na haiwezekani watu walio nchi za mbali wawe kama wao katika hukumu ya kuandama mwezi ikiwa hawakushirikiana nao katika nyakati za kuchomoza kwa mwezi.

Kwa mimi, linalo staajabisha zaidi ni kuwa hoja hii imetoka kwa walio mfano wako, nawe ni katika wanaowazidi wengine kwa akili, na katika wenye hekima katika uoni na maarifa katika Dini. Na kama sikujui kuwa ni mtu mwenye kuheshimika na mwenye cheo kiilimu ningalisema hoja hii haitoki isipokuwa kwa mwenye kuporoja asiyo yajua –hasha kwa wewe-, nami kwa kweli nakuona na heshima yako uko mbali na kushuka hadi daraja hiyo.

Mimi - pamoja na kufuatilia kwangu yale waliyo yasema maulama katika suala hili – sijakuta kamwe kauli ya ye yote kati ya wenye ilmu ya kuupa mwezi wa Dhulhijja peke yake hukumu hii pasina miezi mengine; na atakayeona kauli inayosema hivo kutoka kwa alimu mujtahid ye yote kati ya waliotangulia na waliofuatia basi na aniletee.

FATWA ZA MAULAMA WA SAUDI ARABIA KUHUSU FUNGA YA ARAFA, SALA YA IDI NA KUCHINJA UDH-HIYA

Lilipozuka zogo la watu wasiosoma kuhusiana na hilo na wakadhani rai iliyo sawa imo katika kufunga siku ambayo mahujaji wanasimama huko Arafaati japo ikiwa ni kinyume na uonekano wa mwezi kwao, na kwamba sala ya idi iwe katika siku inayofuatia vyovyote utakavokuwa mwezi umeonekana kwao, maulama walitoa fatwa kuwa hilo si sawa kabisa, na kwamba wao wanatakiwa wazingatie tarehe

ya Dhulhijja kwa mujibu wa muandamo wao, na juu ya msingi huo zinasimama hukumu zote kama ni kufunga siku ya tarehe tisa au kusali idi na kuchinja udh'hiya. Miongoni mwa waliotoa fatwa hiyo ni Sheikh al Allaama Ibnu Uthaimin, na hii hapa ni jawabu yake imenukuliwa kama ilivo:

"Ilivo sawa ni kwamba (funga ya Arafa) inatafautiana kwa kutafautiana nyakati za kuchomoza mwezi. Kwa mfano ukiwa mwezi umeonekana Makka, na ikawa siku hii ni tarehe tisa, na ukaonekana nchi nyengine kabla ya Makka kwa siku moja na ikawa siku ya Arafa kwao ni tarehe kumi haiwajuzii kufunga siku hiyo kwasababu kwao ni siku ya idi. Halikadhalika ingalikuwa kuonekana mwezi kwao kumechelewa kukawa baada ya Makka na ikawa siku ya tarehe tisa Makka ni tarehe nane kwao, watafunga siku ya tarehe tisa kwao ambayo ni tarehe kumi kwa Makka. Hii ndiyo kauli yenye nguvu, kwasababu Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- anasema: 'Mkiuona fungeni na mkiuona fungueni'; na hawa ambao haukuonekana kwa upande wao hawakuwa wameuona, na kama ilivokuwa watu kwa ijmai wanazingatia kuchomoza kwa alfajiri na kuzama kwa jua kila sehemu kwa mujibu wa wakati wake, basi halikadhalika utaratibu wa mwezi huwa kama utaratibu wa siku".(mwsh)

Kauli yake: "Hii ndiyo kauli yenye nguvu" haiashirii kuwepo kauli ya kuupa mwezi wa Dhulhijja pekee hukumu hii, bali anaashiria kauli ya wale walio ifanya miezi yote

utaratibu wake mmoja kwa namna ambayo hutegemea kuonekana mwezi sehemu yo yote duniani ukafuatwa.

Kituo cha Fatwa pia kimeulizwa kuhusu hilo kama nanavonukuu hapa:

"Je tafauti ya nyakati za kuchomoza mwezi inazingatiwa katika idil-hajj? Nini afanye aliyepata mtihani wa kutafautiana waislamu katika mji mmoja katika siku ya idi - je ni Jumamosi au ni Ijumaa? Na kila kundi litasali idi katika siku wanayoiona? Ni nini hukumu katika siku ya Arafa kwa atakayetaka kufunga?"

Jawabu ikawa ifuatavo:

"Sifa njema zinamstahikia Allah na rehma na amani zimshukie Mtume wa Allah na aali zake na masahaba wake. Baada ya hayo:

"Waislamu wanapaswa waache kufarikiana, na washikamane kwa kamba ya Allah wote. Katika hayo ni kwamba watu wa nchi moja yenye wakati mmoja wa kuchomoza mwezi wanalazimika waungane katika kufunga na kuchinja udh-hiya. Yaani wafunge au wachinje katika siku moja kwa kuzingatia kuthibiti muandamo wa mwezi kwao, au kwa kukamilisha siku zote za mwezi, wala haiwalazimu wawafikiane na watu wa nchi nyengine inayotafautiana nao katika wakati wa kuchomoza mwezi."

"Na kwa hiyo, kundi ambalo litasali idi au litafunga Arafa kwa kuthibiti mwezi au idi katika mji huo au miji iliyo jirani nao basi hao ndio ambao inakulazimuni mufunge na musali pamoja nao. Kwani imethibiti katika Sunna alizopokea Abu Daud kwamba Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- kasema: "Kufunga ni siku

mnayofunga, na kufungua ni siku mnayofungua, na kuchinja udh-hiya ni siku mnayochinja udh-hiya"; na muislamu haimjuzii kupinga hilo. Na ikiwa baadhi ya nchi za waislamu zitatangulia au zitachelewa, halizingatiwi lolote kati ya hayo madamu nyakati za kuchomoza mwezi zimetafautiana".

Jawabu hiyo ilikuwa chini ya usimamizi wa Dokta Abdalla Alfaqiih.

Pia kamjibu muulizaji kutoka USA kuhusu suali hilo hilo kama ninavonukuu hapa:

"Sifa njema zinamstahikia Allah na rehma na amani zimshukie Mtume wa Allah na aali zake na masahaba wake. Baada ya hayo:

"Inavotudhihirikia ni kuwa siku ya Arafa kwenu nyinyi ni siku inayotangulia siku ya Idi, kwani ndiyo tarehe tisa kwenu nyinyi. Mfano wa hili ni kama inavokuwa kwa usiku wa Lailatul-Qadri ambao kwenu nyinyi inawezekana ukawa si sawa na Lailatul-Qadri kwa watu wa nchi nyengine. Na funga ya siku ya Arafa ni kitu mbali na kusimama Arafa, kwani funga hii imewekwa katika Sharia kwa asiyekuwa mwenye kuhiji, na kwa hiyo imefunganishwa na wakati siyo na pahala, na wakati kwenu nyinyi ndio unaozingatiwa. Hata hivo kama utafunga Ijumaa na Alkhamisi itakuwa aula, kwasababu Alkhamisi ni tarehe nane, ambayo ni siku ya Tarwiya, na imekuja katika Sharia hukumu ya kuifunga. Na Allah anajua zaidi."

Sheikh Alhaj Muhammad bin Abdil-Wahhab bin Abdir-Razzaq amegusia ghasia za watu wasiokuwa na ilmu

kuhusu hili kwenye kitabu chake "*Al-'adhbu a'Zulaal*" akasema:

"Hili msingi wake ni kuwa kinacho tegemewa katika uonaji wa mwezi ni kuthibiti uonaji wa mwezi Makka, na umeshajua kuwa hilo si sahihi kisharia na kiakili. Pamoja na hayo kama ingalikuwa kinacho kusudiwa katika funga ya siku ya Arafa ni yale aliyosema tu, wasingaliamrishwa kuifunga wale ambao wakati wa alfajiri kwao ndiyo wakati wa kuzama jua kwa watu wa Makka, kwani lazima wakati wa kusimama Arafa ni usiku kwa hawa. Imebainika kwa haya kuwa masuali haya yote yanatokana na kuto kuangalia kwa kina na makini na kuto kusoma maoni ya maimamu wahakiki na wataalamu wa falaki, na kwa hiyo yote ni masuali yasiyo na msingi ambayo haipasi kuyazingatia wala kushughulika nayo kabisa".

Halafu kukaja katika maneno yake mengine kulihisabu jambo kama hilo kuwa ni batili na kwamba linatokana na ukosefu wa ilmu.

KUTAJWA HIJJA PEKE YAKE KATIKA AYA SI HOJA

Ama kauli yako: "Miongoni mwa ambayo yanaupa mwelekeo huu nguvu ni kauli Yake Taala:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ))

[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija] (Albaqara: 189); kwani kutajwa hija pekee baada ya ujumla huu ni ishara yenye nguvu ya kuzingatia msingi wa kuwekwa vipimo vya nyakati kuwa unahusiana na pahala pamoja, napo ni pahala pa nchi takatifu ya Makka tu".

Mimi – pamoja na kustaajibishwa kwangu na hayo pia – sitaki kuyatolea maelezo zaidi kuliko yale waliyosema wafasiri wa Qur'ani kuhusu kutajwa hija pekee. Na nachagua kati yao – baada ya watangulizi wema miongoni mwa masahaba na taabiina na waliowafuatia – wafasiri kutoka Madhehebu Nne, basi pokea yaliyomo katika tafsiri hizo:

1- Kasema Ibnu Jarir a'Tabariy:

'Sema ewe Muhammad, Mola wenu kaweka tafauti hiyo ili kuifanya miezi michanga ambayo mnaulizia na sababu ya kutafautishwa na vinginevo katika yale ambayo ameitafautisha navo ili iwe vipimo vya nyakati kwenu na kwa wengine kati ya wanaadamu katika maisha yenu – ili kwa kuzidi umbo la mwezi na kupungua na kufutika lisionekane kisha mkaliona upya, muangalie nyakati za kulipana madeni yenu, na kumalizika muda wa uajiri wa yule muliye muajiri, na kumalizika eda za wake zenu, na wakati wenu wa

kufunga na wa kufungua; kaifanya miezi michanga iwe vipimo vya nyakati kwa watu.'

'Ama kauli Yake "na Hija" inamaanisha "na kwa ajili ya hija", anasema na kaijaalia pia iwe kipimo cha wakati wa kuhiji kwenu muujulie wakati wa ibada zenu za hija na kuhiji kwenu.'(mwsh)

2- Kasema Ibnu Abi Hatim:

'Katuhadithia baba yangu, kasema katuhadithia Hisham bin Ubaidillah na Musaddad wamesema: Katuhadithia Muhammad bin Jabir kutoka kwa Qais bin Talq kutoka kwa baba yake Talq bin Ali kasema: Kasema Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie: Mwenyezi Mungu kaijaalia miezi michanga iwe vipimo vya nyakati.'

'Kauli Yake: "Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu".'

'Katupa khabari Muhammad bin Sa'd Al Oufiy katika aliyoniandikia, kasema katuhadithia baba yangu, kasema katuhadithia ami yangu Alhusain kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake kutoka kwa Ibnu Abbaas kasema: Watu walimuuliza Mtume wa Allah – rehma za Allah na amani zimshukie- kuhusu miezi michanga ikateremka aya hii:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ))

[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija] Wanajulia kufika kwa wakati wa kulipana madeni yao, eda za wake zao na wakati wa kuhiji kwao.'

'Katuhadithia Isam bin Ruwad, kasema katuhadithia Adam kutoka kwa Abu Ja'far kutoka kwa A'Rabii kutoka kwa Abu Al'aaliya kasema: Imetufikia kwamba wamesema: Ewe Mtume wa Allah kwa nini imeumbwa miezi michanga? Akateremsha Mwenyezi Mungu:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ))

[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija] Anasema: Kaijaalia Mwenyezi Mungu iwe vipimo vya nyakati kwa ajili ya kufunga kwa waislamu na kufungua kwao na eda za wake zao na kufika wakati wa kulipana madeni yao. Na imepokewa kwa 'Ataa na A'Dhahhak na Qatada na A'Suddiy na A'Rabii bin Anas mfano wa hayo.'

'Kauli Yake: "na Hija": Kwa sanad hiyo kutoka kwa Abu Al'aaliya "Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija", anasema: Ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya kuhiji kwao na ibada zao za hija.'

'Na imepokewa kwa A'Dhahhak na Qatada na A'Suddiy na A'Rabii bin Anas mfano wa hayo.'(mwsh)

3- Kasema Ibnu Kathir:

'Kasema Al Oufiy kutoka kwa Ibnu Abbaas watu walimuuliza Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- kuhusu miezi michanga ikateremka aya hii:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ))

[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija] Wanajulia kufika kwa wakati wa kulipana madeni yao, eda za wake zao na wakati wa kuhiji kwao. Na kasema Abu Ja'far kutoka kwa A'Rabii kutoka kwa Abu Al'aaliya kasema: Imetufikia kwamba wamesema: Ewe Mtume wa Allah kwa nini imeumbwa miezi michanga? Akateremsha Mwenyezi Mungu:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ))

[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija] Anasema: Kaijaalia Mwenyezi Mungu iwe vipimo vya nyakati kwa ajili ya kufunga kwa waislamu na kufuturu kwao na eda za wake zao na kufika wakati wa kulipana madeni yao. Na imepokewa kwa 'Ataa na A'Dhahhak na Qatada na A'Suddiy na A'Rabii bin Anas mfano wa hayo. Na kasema Abdu'Razzaq kutoka kwa Abdul'Aziz bin Abi Ruwad kutoka kwa Naafi' kutoka kwa Ibnu Omar kasema: Kasema Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- "Mwenyezi Mungu kaijaalia miezi michanga iwe vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu, basi fungeni mkiuona na fungueni mkiuona; ukizingwa na mawingu msiuone hisabuni siku thalathini". Na Alhaakim kaipokea katika '*Mustadrak*' yake katika hadithi ya Ibnu Abi Ruwad kwa sanadi hiyo, na akasema alikuwa mwenye kuaminika, mwingi wa ibada, mwenye jitihada na mtukufu wa nasaba,

kwa hiyo sahihi kwa sanadi, na wao (Al Bukhari na Muslim) hawakuitoa. Na kasema Muhammad bin Jabir kutoka kwa Qais bin Talq kutoka kwa baba yake Talq kasema: Kasema Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie: "Mwenyezi Mungu kaijaalia miezi michanga iwe vipimo vya nyakati, basi mkiuona mwezi mchanga (umeandama) fungeni na mkiuona fungueni; ukizingwa na mawingu msiuone kamilisheni idadi ya siku thalathini". Na kama hivo imepokewa katika hadithi ya Abu Huraira na katika maneno ya Ali bin Abi Talib –Allah amridhie.'(mwsh)

4- Kasema Alfakhru A'Raaziy:

'Ama kauli Yake Taala: ((وَالْحَجِّ)) "**na Hija**", mna kilicho dhamiriwa bila kutajwa, makadirio yake ni "na kwa ajili ya Hija", kama kauli Yake Taala: ((وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ تَسْتَرْضِعُوا أَوْلَـادَكُمْ)) "**Na mkitaka kutafuta wa kunyonyesha watoto wenu**" yaani kwa ajili ya watoto wenu. Na jua kwamba sisi tumebainisha kuwa miezi michanga ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya nyingi katika ibada, kwa hiyo kutajwa hija pekee lazima mna faida, na haiwezekani ikasemwa kuwa faida hiyo ni kwamba nyakati za hija hazijulikani ila kwa miezi michanga; kasema Taala: ((الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَعْلُومَـاتٌ)) "**Hija ni miezi maalumu**". Na hiyo ni kwasababu wakati wa kufunga pia haujulikani ila kwa miezi michanga, kasema Taala: ((شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ)) "**Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani**".

Na kasema –amani imshukie: "Fungeni mkiuona na fungueni mkiuona". Rai bora kabisa katika hili ni ile aliyoitaja Alqaffaal –Allah amrehemu-: Nayo ni kwamba kutajwa hija pekee kumekuwa tu kwa ajili ya kubainisha kuwa hija wakati wake hauzidi miezi aliyo iainisha Mwenyezi Mungu Taala kwa ajili ya fardhi ya hija, na kwamba haijuzu kuihamisha hija kutoka miezi hiyo kuipeleka kwenye miezi mingine kama walivyokuwa warabu wakifanya hivo katika kucheleweshaa baadhi ya miezi, na Allah anajua zaidi.'(mwsh)

5- Kasema Ibnu Atiyya:

'Na kauli Yake: ((مَوَاقِيتُ)) "**vipimo vya nyakati**", yaani kwa ajili ya kujua wakati wa kulipana madeni na kumalizika kwa eda za wake na kodi na uajiri na mfano wa hayo. Haya ni katika maslahi ya waja, na ni vipimo vya nyakati za hija pia vinavo juliwa wakati wake na miezi yake. Neno *'mawaaqiitu'* halisarifiki kwasababu ni wingi ambao hauna mfano wake katika umoja, na kwa hiyo neno hilo ni wingi na kikomo cha wingi kwani halina wingi wake. Na Ibnu Abi Is'haaq kasoma *walhijju* kwa kasra katika *ha* katika Qur'ani yote na katika kauli Yake *hijjul baiti* kwenye Aal Imraan.'

'Kasema Siibawaihi *alhajju* kama *a'raddu* na *a'shaddu*, na *alhijju* kama *a'dhikru*, hivo ni viini viwili vya neno vyenye maana moja; na kuna kauli kwa fat'ha ni kiini cha neno na kwa kasra ni jina.'(mwsh)

6- Kasema Al Qurtubiy:

'Kaitaja Subhanahu hija peke yake kwasababu ni katika yanayo hitajia kuujua wakati wake na kwasababu haijuzu kucheleweshwa baada ya wakati wake, tafauti na walivoona warabu, kwani wao walikuwa wakihiji kwa kuhisabu idadi ya siku na wakiibadilisha miezi, na Mwenyezi Mungu akaibatilisha kauli yao na matendo yao kama itakavokuja kubainishwa katika surat Bara-a insha Allah Taala.'(mwsh)

7- Kasema Abu Hiyyan:

' "*Walhajji*" (na Hija) imeunganishwa na "*linnaasi*" (kwa ajili ya watu); wamesema makadirio ni "*wa mawaaqiitu lilhajji*" (na ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya Hija), ikaondolewa ya pili kwa kutosheka na ya mwanzo, na maana ni: Ili mujue kwa hiyo miezi michanga miezi ya hija na nyakati zake. Kwa kuwa hija ni katika makuu yanayotafutwa wakati wake na miezi yake kwa miandamo ya miezi ndiyo ikatajwa pekee, kama kwamba ni utajo makhsusi baada ya utajo wa ujumla; kwani kauli Yake: *mawaaqiitu linnaasi*, maana yake siyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya dhati za watu, bali maana yake ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya makusudio ya watu yanayohitajia kupangiwa wakati kidini na kidunia. Kwa hiyo kauli Yake "na hija" imekuja baadae ili kuitaja hija makhsusi baada ya kutajwa kwa ujumla. Hivyo, kwa kweli ibara hiyo haiku unganishwa na "watu", bali imeunganishwa na lile ambalo limenasibishwa kwa "watu" [nalo ni

'makusudio'] ambalo limetolewa na likashika neno "watu" nafasi yake katika irabu. Na ilivokuwa makusudio hayo kuyataja mojamoja kutapelekea kurefusha, katosheka na kauli Yake "ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu".'

'Alqaffaal kasema: Kutajwa hija pekee ni kwa ajiili ya kubainisha kuwa hija wakati wake hauzidi miezi aliyo iainisha Mwenyezi Mungu Taala kwa ajili ya fardhi ya hija na kwamba haijuzu kuihamisha hija kutoka miezi hiyo kuipeleka kwenye miezi mingine; bali warabu ndio waliokuwa wakifanya hivo katika kucheleweshe baadhi ya miezi. Mwisho wa maneno yake.'(mwsh)

8- Kasema Albaghawiy:

'[Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija] (*mawaqiitu*) (vipimo) ni wingi wa *miiqaatu* (kipimo), yaani tumefanya hivo ili watu wajue nyakati za hija, umra, kufunga na kufungua, kuwajibika kulipwa madeni, eda za wanawake na mengineyo; kwa ajili hiyo ndiyo ametafautisha baina ya mwezi na jua, ambalo daima limo katika hali moja.'

9- Kasema Albaidhaawi:

'[Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija]; kwani wao waliuliza kuhusu hekima ya kutafautika hali ya mwezi na kubadilika mambo yake, ndipo Mwenyezi Mungu akamuamuru ajibu kwamba hekima iliyo wazi katika hilo ni ili miezi michanga iwe alama kwa watu wapangie nyakati za mambo yao, pia iwe alama kwa ibada zilizowekewa nyakati ili zijulikane nyakati zake hususan hija, kwani wakati

wake unazingatiwa inapotekelezwa na inapolipwa.' (mwsh)

10- Kasema A'Thaalibi:

'Mwenyezi Mungu ameeleza hekima katika kuzidi mwezi na kupungua na kutafautika kwa hali zake. Tambua kuwa amefanya hivo: ili watu wajue nyakati zao katika hija na umra yao, kufika wakati wa kulipana madeni, na ahadi za walio ahidiana, na ujira wa waajiriwa wao, na kuanza kwa hedhi, na muda wa mimba, na wakati wa kufunga na kufungua na mengineyo. Kwa ajili hiyo katafautisha baina yake na jua, ambalo daima limo katika hali moja.'

11- Kasema Alkhaazin:

'[na hija] yaani na kwa ajili ya hija; na sababu ya kuitaja hija pekee japokuwa imeingia katika jumla ya ibada ni kwa maana kubwa, nayo kwamba warabu katika zama za ujahili walikuwa wakihiji kwa idadi ya siku na walikuwa wakiibadilisha miezi. Mwenyezi Mungu akalibatilisha hilo waliokuwa wakilifanya, na akaeleza kuwa hija haitoki nje ya miezi aliyoi ainisha kwa ajili ya fardhi ya hija kwa miezi miandamo, na kwamba haijuzu kuihamisha hija kutoka miezi hiyo aliyoi ainisha Mwenyezi Mungu Taala kwa ajili yake kama walivokuwa warabu wakifanya kwa kuakhirisha miezi.'(mwsh)

12- Kasema A'Nasafi:

'[Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija] yaani ni alama za watu kupimia nyakati za

vilimo vyao na biashara zao na wakati wa kulipana madeni yao na kufunga na kufungua kwao na eda za wake zao na siku zao za hedhi na muda wao wa mimba na mengineyo, na ni alama kwa ajili ya hija za kuujulia wakati wake.'(mwsh)

13- Kasema A'Naisaburi:

'Na katika kutajwa hija pekee pamoja na kuwa miezi michanga ni alama za ibada nyenginezo pia kama saumu na zakaa, mna ishara ya kwamba hija haitoki nje ya miezi aliyo iainisha Mwenyezi Mungu Taala kwa ajili yake, na kwamba haijuzu kuihamisha hija kutoka miezi hiyo kwenda miezi mingine kama walivokuwa warabu wakifanya hivo katika kuakhirisha miezi.'(mwsh)

14- Kasema A'Samarqandi:

'Anasema hiyo ni alama kwa watu za wakati wa kulipana madeni yao, kufunga na kufungua kwao, eda za wake zao na wakati wa hija yao.'(mwsh)

15- Kasema Jalalu'din A'Suyuti katika "*A'Duraru al-Manthuur*":

'Ametoa Ibnu 'Asaakir kwa sanadi dhaifu kutoka kwa Ibnu Abbaas kuhusu kauli Yake [Wanakuuliza khabari ya miezi michanga], kasema: Imeteremka kuhusiana na Muadh bin Jabal na Tha'laba bin Ghanama, nao ni katika Ansaar, walisema: Ewe Mtume wa Allah! Kwanini mwezi unaonekana unapochomoza mwembamba kama uzi, kisha unazidi mpaka unakuwa mkubwa na kuwa sawa na duara, kisha hauachi kupungua na kuwa mdogo mpaka

unarudi tena kama ulivokuwa, hauwi katika hali moja? Ikateremka:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ))

[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu] za wakati wa kulipana madeni yao, kufunga na kufungua kwao, eda za wake zao na masharti yanayomalizika kwa muda maalumu.'

'Na ametoa Abdu bin Humaid na Ibnu Jarir kutoka kwa Qatada kasema: "Walimuuliza Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie-: Kwa nini ikajaaliwa miezi michanga? Mwenyezi Mungu akateremsha:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ))

[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga] hadi mwisho wa aya. Akaifanya Mwenyezi Mungu iwe alama kwa ajili ya kufunga kwa waislamu na kufungua kwao, na kwa ajili ya ibada zao na hija yao, na eda za wake zao na wakati wa kulipana madeni yao katika vitu mbali mbali, na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kujua zaidi yenye maslahi kwa viumbe vyake.'

'Na ametoa Ibnu Abi Haatim kutoka kwa Abu Al'aaliya kasema: "Tumetajiwa kwamba walimwambia Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie-: Kwa nini ikaumbwa miezi michanga? Mwenyezi Mungu akateremsha:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ))

[**Wanakuuliza khabari ya miezi michanga**] hadi mwisho wa aya. Mwenyezi Mungu kaifanya iwe alama kwa ajili ya kufunga kwa waislamu na kufungua kwao, na kwa ajili hija yao na ibada zao, na eda za wake zao na wakati wa kulipana madeni yao.'

'Pia ametoa Ibnu Jarir kutoka kwa A'Rabii bin Anas mfano wa hayo.

Na ametoa Ibnu Jarir na Ibnu Abi Haatim kutoka kwa Ibnu Abbaas kasema: "Watu walimuuliza Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie- kuhusu miezi michanga, ikateremka aya hii:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ))

[**Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu**] wanajulia wakati wa kulipana madeni yao na eda za wake zao na wakati wa hija yao.'

'Na ametoa Abdu bin Humaid kutoka kwa Mujaahid kuhusu kauli Yake:

((يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ))

[**Wanakuuliza khabari ya miezi michanga. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu**], kasema: kwa ajili ya hija yao, kufunga kwao, kulipana madeni yao na eda za wake zao.'

'Na ametoa A'Tasti kutoka kwa Ibnu Abbaas kwamba Naafi' bin Al-Azraq kamwambia: Nieleze kuhusu kauli Yake: ((مَوَاقِيتُ لِلنَّـــاسِ)) [**ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu**], akasema: Kuhusiana na eda za wake zao, wakati wa kulipana madeni yao na masharti

wanayo wekeana watu. Akasema (Naafi'): Je warabu wanajua hayo? Akasema (Ibnu Abbaas): Naam, kwani hujasikia kauli ya mshairi aliposema:

Na jua latembea kwa wakati limetiishwa
Likimaliza safari laanza upya safari'

'Na ametoa Alhaakim akaisahihisha na Albaihaqi katika kitabu chake cha *Sunan* kutoka kwa Ibn Omar kasema: Kasema Mtume wa Allah –rehma za Allah na amani zimshukie-: "Mwenyezi Mungu kaijaalia miezi michanga iwe vipimo vya nyakati kwa watu kwa hiyo fungeni mkiuona mwezi na fungueni mkiuona; ukizibwa na mawingu msiuone hisabuni siku thalathini.'

'Na ametoa Ahmad, A'Tabari, Ibnu 'Adiy na A'Daaraqutni kwa sanadi dhaifu kutoka kwa Talq bin Ali kasema: Kasema "Mwenyezi Mungu kaijaalia miezi michanga iwe vipimo vya nyakati kwa watu kwa hiyo mkiuona mwezi fungeni na mkiuona fungueni; ukizibwa na mawingu msiuone kamilisheni idadi ya siku thalathini.'(mwsh)

16- Kasema Abu A'Sauud:

'[Wanakuuliza khabari ya miezi michanga] waliomuuliza ni Muadh bin Jabal na Tha'laba bin Ghanama waliposema: Kwanini mwezi unaonekana unapochomoza mwembamba kama uzi, kisha unazidi mpaka unakuwa sawa, kisha hauachi kupungua mpaka urudi tena kama ulivoanza.'

'[Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija], walikuwa wamemuuliza –rehma na amani zimshukie- kuhusu hikma ya kutafautika hali ya mwezi na kubadilika kwake, Allah Mwenye enzi na hikma akamuamuru awajibu kwamba hikma iliyo wazi katika hilo ni ili iwe alama kwa watu katika ibada zao hususan hija, kwani wakati unazingatiwa ndani yake katika kuitekeleza mwanzo na katika kuilipa, vile vile katika maingiliano yao ya kibiashara na mengineyo kwa mujibu wa makubaliano yao.'(mwsh)

17-Kasema Albaqqaai:

'[na Hija], kaitaja hija kwa jina kwa kuwa ni miongoni mwa makuu yanayohusiana na miezi michanga.'

'Kasema Alharraali: Nayo ni mkusanyiko wa waja kwenye kisimamo kimoja katika miezi ya mwisho wa mwaka, kwani hija ni jambo la kidini linaloleta hisia za kumalizika kwa wakati na kutoweka kutokana na yaliyomo ndani yake yanayo ashiria marejeo ya viumbe.'(mwsh)

'Na kwa kuwa hapo zamani walikuwa wamezoea katika hija kufanya maovu, na kwa kuwa watu kuacha waliyo yazoea ni kitu kigumu kabisa kwa nafsi zao, kwa ajili hiyo wamesema Watu wa tariki na Mabwana wa uhakiki: Kiini cha kumkusudia Mwenyezi Mungu Taala ni kuachana na mazoea na kukubali upya mambo yaliyoteremshwa kutoka kwa Msimamizi wa mbingu na ardhi, na kwa hilo ndiyo masahaba -Allah Taala awaridhie- wamekuwa mabwana wa wafuasi wa Uislamu.'(mwsh)

18- Kasema A'Sam'aani:

'Yaani nimefanya niliyo yafanya ili iwe vipimo vya nyakati kwa ajili ya kufunga na kufungua kwenu, na hija yenu, na muda wa kulipana madeni yenu.'

19- Kasema Haqqi:

'Ukisema ilivokuwa miezi michanga ni vipimo vya nyakati wanavojulia watu wote kwa jumla maslahi yao, imejulikana kutokana na hilo kuwa pia ni kipimo cha wakati wa hija kwasababu hija ni miongoni mwa maslahi yanayotegemea wakati, kwa nini ameitaja hija peke yake? Nitajibu kuwa kitu makhsusi yawezekana kikatajwa baada ya ujumla ili kuzindua juu ya umuhimu wake; kwani hija kwa vile katika kuitekeleza na kuilipa unazingatiwa wakati maalumu, kinyume na ibada nyenginezo, ambazo hauzingatiwi wakati maalumu katika kuzilipa.'(mwsh)

20- Kasema Ibnu Aadil:

'Ilivokuwa hija ni katika makuu ambayo hutafutwa nyakati zake na miezi yake kwa miezi michanga, imetajwa pekee.'

21- Kasema Ibnu 'Aashuur:

'Kutajwa kwa faida za kuumbwa miezi michanga katika mnasaba huu ni kwa ajili ya kuashiria kuwa Mwenyezi Mungu ameiwekea hija wakati maalumu katika miezi haukubali kubadilishwa, na hilo ili uwe utangulizi wa kubatilisha yaliyokuwa wakati wa ujahili ya ucheleweshwaji wa miezi ya hija katika baadhi ya miaka.'(mwsh)

22-Kasema A'Nahhaas:

'Akaifanya Mwenyezi Mungu iwe vipimo vya nyakati kwa ajili ya kuhiji waislamu na kufungua kwa waislamu na kufunga kwao, na kwa ajili ya ibada zao, na eda za wake zao na wakati wa kulipana madeni yao, na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kujua zaidi yenye maslahi kwa viumbe vyake.'(mwsh)

Hii ni mifano ya yale ambayo wafasiri wameyasema, na nimeyaona mengi katika yaliyosemwa na wengineo na sijaona popote katika hayo hilo ulilo ashiria wewe katika sababu ya kutajwa hija pekee. Basi sijui unawaona hawakulitaja hilo kwa kutokujua au kwa kughafilika au kwa kusahau?

Na ingawa sitaki kuitolea maelezo hoja yako, ningali nashangazwa na utoaji dalili huu ikiwa kwa mujibu wa mgao wa watu wa mantiki na jumhuri ya wanausuli au kwa mujibu wa mgao wa mahanafi kati yao. Basi je mshangao wangu yawezekana ukaondolewa kwa jawabu yenye ponyo?

HITIMISHO

Baada ya ubainisho huu na maandiko niliyo yataja ya wanavyuoni wa fiqhi wa Madhehebu Nne, je inabaki shaka kwamba msimamo wetu haukuwa na msingi wa kimadhehebu? Kwani wewe unaniona sijataja hata herufi moja katika yale waliyo yasema wanavyuoni wa fiqhi wa madhehebu yangu, bali nilijitahidi kuwarudisha wenye shaka juu ya suala hili kwenye yale wanayo yasema wanavyuoni wao wa fiqhi. Sijui kama wanavyuoni wa fiqhi hawa pia wanatuhumiwa kama mimi kuwa wametegemea msingi wa upendeleo wa kimadhehebu katika waliyo yasema! Hata hivyo, katika kufuata kauli hii – na Allah ndiye wa kushukuriwa – hatukuwa sisi peke yetu, bali pengine tukiangalia walio wengi kabisa katika waislamu tutawakuta wanashiriki katika kuwa na msimamo huu huu. Nchi ya Moroko, mataifa ya Afrika ya Mashariki yote, Turkia, Irani, India, Pakistani, Bangladeshi na nyingi za nchi za Afrika ya Magharibi na za Asia ya Mashariki zinafuata mfumo huu huu. Je uko wapi ushabiki wa kimadhehebu katika hili?

Pamoja na haya yote, mimi niko tayari kabisa kupokea maoni yo yote juu ya nukta yo yote katika jawabu hii; kwa hiyo iangalie kwa makini na tafuta msaada wa unayetaka kati ya wanavyuoni wa fiqhi sawa ikiwa kutoka ndani ya Oman au nje yake. Na nitafurahishwa pia iwapo itafanywa hivo na kila atakayeisoma jawabu hii, na ingependeza mno kama

mtaionesha kwa maulama wa Saudi Arabi kutokana na kuwa wao wanahusika zaidi na jambo hili, kwa kuwa ni wasimamizi wa Misikiti Miwili Mitukufu, na nawataja makhsusi kati yao Kamati ya Kudumu ya Utafiti na Fatwa, Baraza la Wakubwa wa Maulama, hususan Mstahiwa Sheikh Dokta Ndugu Saleh bin Abdalla bin Humaid – Kiongozi wa Ukadhi Mkuu, kwani yeye kwa wadhifa wake huu anahusika mno na masuala ya miandamo ya mwezi.

Nami kabisa sioni tabu kuacha lolote ambalo nimelisema ninapo kinaishwa na ye yote kuwa ni batili au ni kosa kwa dalili iliyo wazi. Lakini napinga vikali kufuata hisia za mapenzi na chuki za kijuha na ikawekwa kando dalili. Kwani Mwenyezi Mungu hakuzihusisha kabisa hisia za watu na masuala ya Dini, bali Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala hakuzijaalia akili kuhukumu katika yanayohusu Sharia Yake; kwa hiyo hukumu hapana budi itafutwe katika Sharia Yake safi. Kisha Mwenyezi Mungu Subhanahu kabainisha nani ambao kwao inatafutwa hukumu pakiwa na mzozo na kutafautiana aliposema:

((فَإِنْ تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا))

[Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema] A'nisaa 59.

Wanavyuoni wa fiqhi waliobobea katika ilmu ndio ambao inawajibika watakwe msaada katika kufichua

yaliyofichika na kutanzua yaliyotanzika kutokana na dalili za Sharia ili kutekeleza kauli Yake Taala:

((وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَى الرَّسُولِ وَإِلَى أُولِي الْأَمْرِ مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنْبِطُونَهُ مِنْهُمْ))

[**Na lau wangeli lipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wale wanao chunguza wangeli lijua**] A'nisaa 83.

Hivyo, haijuzu kuvutiwa na wanayo yasema watu wa kawaida wasiokuwa na ilmu, ambao hawatafautishi baina ya kenge na nyangumi wala baina ya mbwa mwitu na mwana wa kondoo; vipi hawa wataweza kuzamia kwenye vina vya bahari ya Sharia wakatoe lulu za hukumu za Sharia?

Nawe ewe Sheikh kutokana na nafasi yako ya kielimu na hadhi yako kijamii unastahili kuwa na hima ya kuwaonesha watu wa kawaida njia za salama; kwani hili ni jukumu lako mbele ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu amechukua juu yako ahadi ya kubainisha. Hivyo ni juu yako kubainisha, na zisikuzuie katika hilo lawama za mwenye kulaumu, wala haikujuzii baina yako na Mola wako kuendeshwa pamoja nao na hisia za mapenzi na chuki, kwani hilo linapelekea kwenye fujo ambayo mwisho wake hauwi mwema. Na hapana shaka kuwa katika kila madhehebu – bila kuacha yoyote – kuna kundi la wasiokuwa na ilmu wanaojipa kujua; hao ni mtihani kwa madhehebu zao, msiba kwa wanavyuoni wao wa fiqhi na mzigo juu jamii zao. Utamuona mmoja wao kutokana na mwisho wa ujuha wake hatafautishi baina ya sehemu ya mbele na ya nyuma

ya farasi, huku anajiona ni alimu kuliko sahibu yake Musa – amani imshukie-, na mwenye hikma kuliko Luqman, na mhutubu kuliko Qis, na fasihi kuliko Sahban, na mvumilivu kuliko Al-ahnaf; kwasababu tabia ya kujiona ni umbile katika kila nafsi ikiwa haikutakaswa kwa ilmu na tabia njema. Na ni katika tabia ya watu wajinga kupenda kujionesha kuwa wanajua na kujipa ufasaha mbele ya maulama:

Kila mmoja adai kuwasiliana na Laila
Ilihali hilo hawakubalii mwenyewe Laila

Na zamani kulisemwa, "Mjinga angenyamaza, mwenye akili angepumzika."

Na mwenye kupekua katika kurasa za historia akaangalia kwa makini hikima ya wanafasihi atakuta malalamiko haya kutoka kwa wengi miongoni mwa watu wa fiqhi na fasihi, kama ilivo katika kauli ya mmoja kati ya wanafasihi isemayo:

Daraja ya faqihi kutoka kwa alo safihi
Kama daraja ya safihi kutoka kwa faqihi
Kwani huyu hana haja ya ukaribu wa huyu
Na huyu hana haja kabisa ya kuwa na huyu
Uovu ukimzidi yule aliye safihi
Hujipa ufasaha kumpinga alo faqihi

Hili linamaanisha ongezeko la majukumu ya wenye ilmu katika kuwaonesha haki watu wasiosoma; kwani mfano wa wenye ilmu ni mfano wa madaktari. Tafauti

pekee baina ya hawa na hawa ni kwamba madaktari kazi yao ni kuganga miili, wakati maulama kazi yao ni kuganga akili na nyoyo. Na kwa hiyo wao wanahitaji zaidi hekima na wanastahili mno kuwa na subira juu ya mashaka ya wagonjwa wao na ukaidi wao.

Na wewe ewe Sheikh hayakufichikii haya; inakutosha kwamba wewe umri umekupa busara ukakujuvya shida na raha, ukatoka na chumo la uzoefu unaokutosha uwe kwako ni busara na muongozo, achilia mbali kadiri uliyochukua katika ilimu ya manufaa na yale unayosifika nayo katika tabia tukufu. Mtu mfano wako ni wa kutegemewa katika utatuzi wa matatizo yaliyo makubwa kuliko haya, na kwa hiyo haikupasi uogope kuyaingia, kwani hekima ya wenye hekima ndiyo ponyo la papara ya wasiosoma na ujuha wa majuha. Basi muombe Allah akusaidie katika kutimiza amana aliyo kubebesha, na kichukue Kitabu kwa nguvu; Allah akufanikishe kwa kila lenye kheri, na akusaidie katika kila jema na la uongofu, na akuhifadhi na kila ovu, nawe unastahiki shukrani nyingi, heshima, usafi wa moyo na utajo mwema.

Ndugu yako aliyekusafia moyo,
Ahmad bin Hamad Al Khalili
8 /Dhulhijja/ 1430AH